**Paulo Analeta Habari Njema na Mungu Ulimwenguni**
**Matendo Sehemu ya 2, Sura ya 13-28**

| | |
|---|---|
| • **Safari tatu za kitume za Paulo tokea Antiokia**<br>• **Kuhubiri kwa nguvu za Roho Mtakatifu kuanzisha Makanisa mapya**<br>• **Miujiza, upinzani na mateso** | • **Kufundisha na kutuma barua ili kuhimiza Utakatifu**<br>• **Kukamatwa Yerusalemu, na Merikebu iliyovunjika Melita**<br>• **Mfungwa wa Kristo Rumi** |

**KITABU HIKI** kiknafafanua sehemu ya pili ya Kitabu cha Matendo ya mitume, na safari tatu za ki utume za Mtume Paulo Rumi miaka 2000 iliyopita. Mafundisho ya Paulo yalisambaa haraka katikja Rumi kwa sababu ya barua zao na kuhubiri, zinabaki kama miongozo kwa mamilioni ya wakristo leo. Kielelezo chake, hutuhimiza waanini kumfuata Yesu ba Kristo maisha ya utauwa katika ushirika wa mapendo na waamini wengine.

**SHIRIKA LA CHAPA LA MANNA** inasambaza Biblia zilizoandikwa na Fred Morris. Kwa miaka mingi, Fred pamoja na mkewe Lorna, wanasasafiri Duniani wakihubiri na kufundisha, na waliporudi, Fred aliakili maandishi haya, kwa ajili ya kucyhapa na kuyyza popote palionekana na uhitaji wa mafundisho ya msingi ya Kristo.

**FASIHI ZA MAFUNDISHO YA BIBLIA** ni rahisi kusoma, rahisi kuelewa na rahisi kutafsiri katika Lugha nyingine.

**VITABU HIVI** ni vya kutumia binafsi au kujifunza katika vikundi, vitakusaidia kujiua kweli ya Mwenyezi Mungu ajulikane Kiebrania kama YAHWEH. Anaabudiwa na Wayahudi pamoja na Wakristo. Biblia mbili ulimwenguni, Vitabu hivi vitakusaidia kupokea wokovu na uzima wa milele kupitia Yesu Kristo Masihi Mwana wa ugu anbaye Kiebrania anajulikana kama YESHUSA vitakusaidia kuzungumza Imani yako kwa Mungu na kuomba. Vitakuongoza dhidi ya njia mbaya ikatika maisha. Vitakusaidia kuishi maisha yanayopendeza Mungu.

**TUNAOMBA** uwe Amani mpya na kusudi jipya katika maisha kadri unavyomuani Mungu, usome Biblia na utumie fasihi hizi za Biblia. Kadri usomapo fikiria ikile Yesu alisema na kufanya miaka 2000 iliyopita kwa ajili ya ukombozi wake na kipi anakuitia useme na kufanya leo ili kuandaa njia yaje hata ajapo.


## Shirika la Chapa la Manna

**FASIRI ZA MAFUNDISHO YA MSINGI YA BIBLIA**


**"Ninyi mmejaliwa Kuzjua Siri ya Ufalme wa Mungu" (Marko 4:11)**


# Paulo Aleta Habari Njema Kwa Ulimwengu

# Matendo Ya Mitume

**Fasiri ya kufundisha Biblia kwa kujifunza binafsi au kwa kikundi Fred Morris**

**Kimetafsiriwa na Pastor Festus Kija Ikoba na Gervase Martin Masanja**




## Matendo Sehumu 2
## Sura 13 hadi 28

Manna Publications

**Kwa Msomaji au Kiongozi**

Vitabu hivi vya fasiri vinasaidia kuieleza Biblia katika njia rahisi kuisoma na kuielewa. Pia ni rahisi kutafsiri. Unaweza kutumia vitabu hivi kujifunza peke yako au pamoja na wengine kwenye kikundi. Kila mmoja sharti awe na kitabu chake; kama inawezekana.

**Kusoma Biblia:** Unapoona maneno haya, inamaanisha wewe au kiongozi wa kikundi lazima kusoma kifungu cha Biblia kilichotajwa kwanza kabla ya kusoma kitabu hiki.

**Jifunze hili:** Unapoona hili, maneno yatakusaidia kutazama mambo muhimu kujua na kushirikisha wengine kuwasaidia kukua katika elimu ya Biblia na kuelewa kweli ya Mungu.

**Zungumza kuhusu hili: -** Unapoona maneno haya kuna maswali ya kujibu wewe binafsi baada ya kuomba au kujadiliana katika kikundi. Pia humsaidia msomaji kuikumbuka mistari ya Biblia.

**Fikiri kuhusu hili:** Unapoona maneno haya, kuna swali linalohitaji muda wa kutafakari kwanza, kabla ya kujibu.

**Vikasha vya kufundishia:** Unapokiona hiki, hutoa habari zenye mafundisho zaidi juu ya mada maalum kwa wanafunzi, waalimu na wachungaji ambayo yanayowafaa wakristo leo.

**Shukrani:** Nukuu ya mistari ya Biblia, kutoka BIBLIA TAKATIFU, Swahili Union, © mwaka, Chama Cha Biblia, Cha Tanzania S.L.P 175, Dodoma, Tanzania na, Chama Cha Biblia cha Kenya. S.L.P 72983-00200, Nairobi, Kenya. Mtayarishaji wa Chapa: Chama cha Biblia Cha Korea, 2017

Picha ni hakimiliki © Global Recordings Network (GRN). Inatumika kwa ruhusa.

---

**Matendo Sehemu ya 2. Fasiri za kufundishia Biblia za Manna, ©2005,2012,2019 Fred Morris, Machapisho ya Manna (USA). Inc. Haki zote zimehifadhiwa**

**Mungu ametuwezesha kuchapa jina hili katika nchi zifuatazo:**

***Revised Worldwide English edition first published in the UK in 2005***

Reprinted 2005 in Uganda (English)
Reprinted 2006 in Myanmar (English)
Reprinted 2008 in Myanmar (Tiddim Chin); Liberia and Sierra Leone (English); Kosova (English/Albanian)
Reprinted 2009 in Nigeria and Uganda (English); D.R. Congo, Katanga (Kiluba and French); Pakistan (Saraiki)
Reprinted 2010 in D.R. Congo, Katanga (Kisongye and French), in Malawi (Chichewa Braille), Cameroon (French and English) and UK and Liberia (English)
Reprinted 2011 in India (Telugu), Pakistan (Saraiki), Cameroon (English), Myanmar (Dai) and Mozambique (Portuguese), India (Telugu and English), Guatemala (Spanish)
***Second edition*** published 2012 in India (English, Telugu and Tamil), Cameroon (English and French)
Reprinted 2013 in D.R. Congo, Katanga (Kiluba and Portuguese), Myanmar (Falam Chin)
Reprinted 2014 in D.R. Congo, Katanga (French, Kiluba), Ethiopia (Oromo)
Reprinted 2015 in Malawi (Chichewa Braille, English, Braille), D.R. Congo, Katanga (French, Portuguese), Cameroon (English), Ethiopia (Amharic, Oromo)
Reprinted 2016 in Ethiopia (Oromo), Cameroon (English), Malawi (English Braille)
Reprinted 2017 in Myanmar (Falam Chin, Ngawn Chin), Cameroon (English)
Reprinted 2018 in Myanmar (Ngawn Chin, Falam Chin), R.D. Congo, Kinshasa (French), Cameroon (French)
Reprinted 2019 in Myanmar (Ngawn Chin)
Reprinted 2020 in Cameroon (French)
***Third edition*** published 2021
Reprinted 2023: Kenya (English), D.R.Congo, Katanga (Swahili).
Reprinted 2024: Kenya (Swahili)

**Imechapwa na:**
Manna Publications (UK)

**Imechapishwa na:**
MissionAssist (UK)

**Kusambazwa na:**
Word of Life School of Theology Ltd
P.O. Box 115
Kianjai 60602
Meru, Kenya
Tel: +254 (0)727 898 897

**Kwa kushirikiana na:**
New Dawn Ministry, Meru and
Pastor Fred Mugambi Iburi, Isiolo

**Mechapwana na:**
Pencam Vision Printers
Meru, Kenya

**Mungu amewezesha fasihi za Biblia za Manna Kuchapishwa:**

Angola, Armenia, Benin, Burkina Faso, Cambodia, Ginorea, Chad, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Kinshasa na Katanga) Jamhuri ya Congo (Brazzaville), Egaatorial Guinea, Ethiopia, Ghana, Guantamala, Haiti, India, Ivory Coast, Kenya, Kosovo, Liberia, Malawi, Mali, Mexco, Mongolia, Msumbiji, Myaar, Nepal, Niger, Nigeria, Pakistan, Rwanda, Serbia, Sierra Leone, Afrika Kusini, Sudan, m Swaziland, Tanzania, Togo, Uganda. Zambia na Zimbabwe.

**Na katika Lugha 43 na 2 za Breli (Lugha za alama kwa wasioona)**

Tembelea tovuti yetu katika **www.manna-publications.org.uk** kwa ufafanuzi zaidi wa mafundisho ya Biblia kwa Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kihispania. Tafadhali wasiliana nasi kupitia tovuti yetu kwa lugha zingine.

Pia kwa Kifaransa, Kireno na Kihispaniola

linalohusisha na **Avail** asasi iliyosahiliwa kwa namba 1017386

Shirika Mama **Manna Publication (USA)**

wa kitabu cha Waebrania. Waamini walifarijiwa na wakaimarishwa kwa kusoma AGANO JIPYA, pamoja na hali za kukunja za Agano la Kale.

Tunaweza kuamini maneno ya waandishi wa Agano Jipya kuhusu Yesu na mafundisho yake, kwa kuwa wote walimjua Yesu kibinafsi. Yesu mfufuka alizungumza na Paulo na kumtuma awe shahidi wake ulimwenguni.

Hivyo tunamshukuru Mungu kwa ajili ya barua za Paulo na za wengine zinazomfundisha kila mmoja kweli kuhusu Yesu Kristo ambaye ni Mwana wa Mungu. Ni jambo jema kwa kila muumini kusoma barua za Paulo na barua zingine za Agano Jipya zaidi kitabu cha Matendo ya Mitume. Ni kitabu muhimu sana hasa kwenye kipindi cha kukua kwa Kanisa, kufa kwa Kanisa, Mateso ya Kanisa hususani Injili zote nne zilizo sheheni Maneno na Huduma ya Yesu Mwenyewe.

Watu wengi wanaamini kwamba tuko karibu na wakati wa matatizo makubwa hapo awali Kristo anarudi (Mark 13:4-8). Watatilia mashaka Imani zao. Wengi watadanganywa na viongozi wenye Nguvu na ushawishi na Imani (dini) zingine. Lakini wengi wataokolewa na kubaki thabiti kwa Mungu kwa kutii mafundisho ya Yesu Kristo na Mitume wake tunaposubiri kuja kwake.

Kanisa la Antiokia huko Siria lilimtuma Paulo na wengine kwenda kuhubiri Habari Njema za Yesu Kristo. Makanisa madogo mengi yalianzishwa huko Rumi. Nayo pia yalituma wahubiri na Mitume ulimwenguni kote.

**Maombi:** Baba yetu wa Maombi, unganisha na kuwawezesha watu wako ili kweli yako iendelee kuufikia ulimwengu. Thibisha wokovu wako wa milele na Haki kupitia Yesu Kristo, aliyetolewa kama dhabihu ya Bwana Mungu wa Wayahudi na Wakristo kote. Ufalme wako uje duniani kana huko mbinguni, Utujie Bwana Yesu.

[Acts Part 2 Swahili, 3rd edition, 2021, revised 2024]



# Matendo Sehemu 2: Sura 13-28

## UTANGULIZI

Hii ni sehemu ya pili ya Mafundisho ya Biblia yenye fasiri ya Machapisho ya Manna, yaliyoandaliwa na Fred Morris kwa ajili ya kufundisha Kitabu cha Matendo ya Mitume.

"Matendo" ni moja kati ya vitabu viwili vya Agano Jipya vilichoandaliwa na Luka, aliyekuwa rafiki wa karibu wa Mtume Paulo. Luka aliandika kitabu hiki mwishoni mwa karne ya kwanza baada ya maisha, kifo, kufufuka na kupaa kwa Yesu Kristo Mwana wa Mungu.

Kitabu cha Matendo kiliandikiwa wafuasi wa "Njia Ile", walioiamini Habari Njema na pia kumwamini Yesu ambao baadaye walijulikana kama "wakristo".

Kitabu cha Matendo kinaelezea mambo yaliyowapata Wayahudi walioamini pamoja na waumini wengine na jinsi ushuhuda wao ulivyobadilisha ulimwengu kama Yesu mwenyewe alivyoaahidi (1:8).

Katika kitabu chetu cha kwanza cha fasiri cha Matendo ya Mitume, tunasoma kuwa **Yesu** (jina la Kiebrania ni **Yeshua**) alirudi mbinguni kuwa na Baba yake ambaye ni Muumbaji na Mungu Mwenyezi (Jina la Kiebrania **Yahwe).**

Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu wake atakuwa pamoja na wafuasi wake. Jambo hili lilitokea kule Yerusalemu siku ya Pentekoste kupitia nguvu za Roho, Mungu aliwawezesha wale wafuasi 120 wa Yesu kuongezeka idadi kila siku na kufikia maelfu.

Roho Mtakatifu aliwatia moyo wanafunzi au mitume wa Yesu kuhubiri kwa ujasiri Habari Njema za Yesu. Pia Roho aliwawezesha kuponya wagonjwa kwa jina la Yesu.

Neno' mtume' linamaanisha mjumbe. Neno "mwamini" maana yake "mtu anayemwamini Mungu, na ni mfuasi wa Yesu Kristo, anayeamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu".

Kupitia kuhubiriwa Habari Njema na kazi ya Roho Mtakatifu, maelfu ya watu waliamini na kuokolewa na hukumu ya Mungu.

Walibatizwa na kuanza maisha mapya ya imani kwa Mungu. Walipokea haki na ahadi yake ya uzima wa milele pamoja na Yesu.

## MYAHUDI ALIYEITWA SAULI

Hapo kwanza ni Wayahudi tu ndio waliosikia Habari Njema. Wengi walimwamini Yesu kama Mwana wa Mungu, Masihi wao wa Kiyahudi, yaani Kristo. Aliahidiwa na Mungu miaka mingi kabla ya kuandikwa kwenye Agano la Kale, kwenye hati za kukunja kwa kuviringishwa.

Waumini wapya walikutana na wafuasi wa Yesu wa kwanza, wakachanganyika na Wayahudi katika baraza ya Hekalu la Yerusalemu na katika masinagogi ya Kiyahudi popote duniani.

Baadhi ya viongozi wa Kiyahudi walipinga mafundisho ya mitume. Kiongozi mmoja wa Kiyahudi alipewa ruhusa kuwakamata na kuwaweka wafuasi wengi wa Kristo gerezani. Baadhi yao waliuawa. Lakini siku moja Mungu alimzuia asifanye hivyo. Yesu alimsamehe Sauli akiwa kwenye barabara iendayo Dameski (9:3-6). Naye pia, akawa mfuasi wa Yesu. Yesu alipomsamehe alipokea nguvu za Roho Mtakatifu (9:17-19) za kuhubiri Habari Njema za Yesu Kristo. Sauli huyo baadaye aliitwa Paulo kwa jina la Kirumi.

Katika kitabu cha fasiri ya Matendo, tunakuambia kuhusu maisha na safari zake, (Paulo) za kimishenari. Paulo baadaye alitoka kwenye kanisa la Yerusalemu na kuhamia kanisa la ulimwengu kule Antiokia-ya-Syria. Aliuzungukia ulimwengu (wa wakati huo) akihubiri kwa nguvu za Roho Mtakatifu, akisema kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, aliyekuja duniani ili atuunganishe na Baba yake. Paulo alifundisha kwamba alimruhusu Yesu kupokea adhabu kwa ajili ya dhambi zetu ili tuweze kusamehewa. Ujue kwamba tukimwamini Yesu na kumfuata, tutaishi pamoja Naye milele baada ya kufariki (1 Thes. 4:13-18).

Sauli (Paulo kwa Kirumi) hapo mwanzo hakuweza kuyaelewa mambo hayo, sawa na sisi leo. Baada ya kusoma maandiko ya Agano la Kale kwenye hati za kukunja na kurudia tena na tena, Paulo aliweza kuamini kuwa lilikuwa kusudi la Mungu kuwaokoa watu ulimwenguni kote kwa kutoa wokovu kwa ajili ya watu wote kupitia Yesu Kristo. Kama nasi tutasoma Biblia zetu kila siku, Roho Mtakatifu atatusaidia kuyaelewa mambo haya.

Sauli alikuwa analielewa Agano la Kale vizuri sana. Maandiko yanaeleza kuhusu Masihi ambaye Mungu angemtuma kwa Wayahudi. Baada ya kuokolewa Sauli aliamini kuwa Yesu ndiye Masihi wa Mungu au Kristo. Pia aliamini zaidi kuwa Yesu alikuja kuwaokoa hata watu wengine ambao hawakuwa Wayahudi. (yaani watu wa mataifa mengine) sawa tu na Wayahudi. Ndiyo maana akayatenga maisha yake kueneza ujumbe au Habari Njema za Yesu Kristo.

Sauli alisikia na kuelewa mafundisho yote ya Yesu kupitia baadhi ya mitume walioishi na Yesu. Alijadiliana juu ya Habari Njema na Wayahudi na Wamataifa (wasio Wayahudi) katika himaya ya Rumi yote. Huo ndio ulikuwa mpango wa Mungu na kusudi lake (9:15). Sauli aliandika nyaraka nyingi kwa makanisa aliyoyapanda nchini Kipro, Uturuki, Ugiriki, Italia na mahali pengine.

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 13

**Jifunze kuhusu:** *Kazi ya Roho Mtakatifu katika Kanisa la Antiokia (1-3); jinsi liwali wa Kipro alivyomwamini Yesu (4-12); jinsi Sauli alivyohubiri Habari Njema kwa Wayahudi waliokuwa Antiokia ya Pisidia (13-41); jinsi watu*



utayari wa kuja na kusikiliza na kupitia nyaraka za Paulo za gerezani; makanisa yalitiwa moyo kwa kupewa ufafanuzi wa mafundisho Kristo na kusudi la Mungu kwenye Agano la Kale.

Paulo alikuwa na ujasiri kwamba Habari Njema za Wokovu wa Mungu katika Yesu zitahubiriwa katika mataifa yote. Alisema, "watasikia"

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Wamiliki wa Merikebu waliwezaje kufanya makosa (27:9-12)? Mungu alifanyaje kumtumia Paulo kuokoa maisha ya watu kwenye meli?
2. Mungu aliwezaje kumtumia Paulo kuokoa maisha ya watu ndani ya Merikebu?
3. Kwa jinsi ya namna gani Mungu alimhimiza Paulo kuelekea Rumi kama mfungwa? (28:14-15; 27:23-25).
4. Jadili ni kwa jinsi gani Paulo alibadilisha maisha ya watu huko Melita (28:2-10)?
5. Kwa jinsi gani Mungu alimtumia Paulo hali akiwa mfungwa Rumi (28:17-30)?

**Fikiria kuhusu hili:** Kwa jinsi gani Mungu alikamilisha mpango wake wa kulijenga Kanisa katika siku za mwisho za uhai wa Paulo? Ombea imani ya kuendelea kumwamini Mungu katika masumbuko ya maisha na kuenezwa kwa Habari Njema. Je, unaanza kuona jinsi Mungu alivyofanikisha shauku ya Paulo kufundisha na kuhubiri Habari Njema Rumi na jinsi gani kuwa mfungwa wa Kristo kulivyokamilisha kusudi la Mungu? Je, huwa unamuomba Mungu akuongoze kila siku?

## HITIMISHO

Huko Rumi Paulo alikuwa katikati ya nyumba ya Rumi. Kwa sababu hii Habari Njema za Yesu Kristo zilienea kote ulimwenguni. (Wafilipi 1:12-14). Hii ilitokea kwa sababu akiwa Rumi Paulo alizungumza na wageni wake na akayaandikia makanisa yake. Wito wa Paulo kwenye huduma ulitimiza maneno ya Yesu mwenyewe (9:15-16; 23:11) ya kuhubiri kwa Wayahudi, mataifa hata kwa Wafalme.

Yesu aliwaonya wafuasi wake "kila mtu atawachukia kwa ajili yangu". Lakini yule atakae simama imara (kuvumilia, kvj) mpaka mwisho ndiye atakayeokoka (Marko 13:13). Hivyo Paulo alisimama imara mpaka kazi yake, aliyopewa na Mungu ilipokamilika. Kuna uwezekanao wa Paulo kuuawa na mfalme Nero (mwaka 67 baada ya Kristo). Hii ilikuwa ni baada ya safari tatu za kimishionari, mapigo mengi, kufungwa na vitisho dhidi yake, na ile safari hatari ya Rumi.

Wakati wa miaka iliyofuata baada ya kifo cha Paulo Maandiko ya Luka (injili ya Luka na kitabu cha Matendo ya Mitume) yalinakiliwa mara kadhaa na kupewa waamini wasome. Hii ilitokea pia kwenye Nyaraka za Mathayo, Marko, Yohana, Petro, Yakobo na barua za Paulo na mitume wengine, na mwandishi

"Lazima atakuwa muuaji", watu walisema wakisubiri afe kwa sumu ya nyoka huyo lakini hakuna kilichotokea, wakasema tena alikuwa ni mungu (28:6).

Mtawala Mkuu wa Rumi wa Kisiwa cha Malta akawachukua Paulo na rafiki zake nyumbani kwake. Baba yake alikuwa mgonjwa, amelala kitandani hivyo Paulo akamwombea na kumwekea mikono Mungu akamponya. Wagonjwa wengine wengi wamjia Paulo kwa maombezi na kuponywa (28:8-9).

Wakati Paulo akikaa huko, kisiwa chote cha Malta walipata fursa ya kusikia kuhusu Yesu. Ukristo katika Malta ulianzia kipindi hicho, mara nyingi Malta ilishambuliwa na mataifa yaliyokizunguka. Lakini watu wa Malta walimwamini Mungu kwa uhuru wao.

Miezi mitatu baadae Paulo alichukuliwa kwenda Rumi kwa meli. Dhoruba za wakati wa baridi zilikuwa zimekwisha. Kabla ya kufika katika jiji la Rumi, waamini wenyewe walikuja kumuona, naye aliwatia moyo na kumtukuza Mungu (28:15).

## HUDUMA YA PAULO RUMI

Miaka miwili Paulo alikuwa chini ya kifungo cha nje akiwa nyumbani kwake, katika nyumba aliyopanga, na kuwakaribsha wote waliokuja kumwona (28:30).



**Paulo asubiri Rumi ka Mfungwa**

Paulo aliezea ufalme wa Mungu kwa Wayahudi walioishi huko. Alitumia vitabu vya Torati ya Musa na Manabii, kuwafundisha. Alisema nao kuhusu Yesu na kufufuka kwake pia (28:23).

Baaadhi yao waliamini Habari Njema lakini wengi walikataa. Ndipo Paulo alitumia maneno ya Isaya (Isa. 6:9-10) ambayo Yesu aliyatumia pia (Mt. 13:3-23), Mk. 4:3-20, Lk 8:4-15).

Luka hatuelezi wazi nini kilitokea baadae kwa Paulo. Lakini tunaamini aliuawa kipindi cha Nero kulikuwa na adha kuu iliyowakuta wanafunzi wa Kristo.

Angali Rumi Paulo alihubiri Habari Njema za Yesu Kristo kwa ujasiri (28:31). Aliandika barua kwa baadhi ya makanisa ya kwanza ya huduma yake. Ilikuwa ni muhimu Paulo kuwafundisha. Nyaraka zake zinasaidia pia kuwafundishia waamini siku za leo, kama ziada ya mafundisho ya Yesu katika vitabu vya injili.

Shauku ya Paulo kwenda Rumi ilitimizwa kwa jinsi ya ajabu. Mungu aliruhusu aende kule kama mfungwa wala si kama mtu huru. Alikuwa mfungwa kwa ajili ya Kristo. Kwa jinsi hii habari njema ilihubiriwa kwa wale walikuwa na



*walivyoyapokea mahubiri ya Sauli (42-45,48-50,52); jinsi Sauli na Barnaba walivyowajibu wapinzani (46-47,51).*

## SAFARI YA KWANZA YA SAULI KUHUBIRI HABARI NJEMA ZA KRISTO

Wayahudi na Wamataifa waliomwamini Kristo waliitwa wakristo kwa mara ya kwanza katika kanisa la Antiokia (11:26) liliongezeka nguvu. Mji wa Antiokia ulikuwa katika nchi ya Syria, kilometa 500 kaskazini kutoka Yerusalem. Kati ya viongozi waliokuwepo ni Barnaba, Simoni, Lukio, Manaeni na Sauli. (13:1-2). Pia kijana Yohana Marko aliabudu katika kanisa hilo, na huyo ndiye aliandika Injili ya Marko baadaye (13:5). Baadhi yao walikuwa waalimu, wahubiri, na wengine walikuwa na kipawa cha unabii. Kufundisha, kuhubiri na kutoa unabii vyote ni vipawa vya Roho Mtakatifu, aliwapa wale aliowachagua Mungu.

Siku moja walivyokuwa wakiabudu, kuomba na kufunga, Roho Mtakatifu alisema na waamuni akawaambia, "Nitengeeni Barnaba na Sauli, kwa kazi ile niliyowaatia" (13:2).



**Wazee wa Kanisa wakiwaombea Sauli na Barnaba**

Viongozi wa Kanisa wakafunga tena, na kuwaombea Barnaba na Sauli, na kuwawekea mikono juu ya vichwa vyao, na kuwaacha waende zao na kufanya kazi maalumu ambayo Mungu aliwaaitia (13:3). Roho Mtakatifu alikuwa anadhibiti mambo yote, akawaita na kuwaongoza watumishi wake. Aliwatangulia kuiandaa mioyo ya watu watakaosikia Habari Njema ili wapokee imani.

Hebu fahamu mambo haya kuhusu wito wa Sauli na Barnaba: -

- Sauli na Barnaba walikuwa viongozi walioaminiwa na kanisa wakati huo (13:1).
- Walitoa muda ili kumruhusu Roho Mtakatifu aseme na kanisa kupitia watu (13:2).
- Manabii na walimu walifunga na kuomba uongozi wa Roho Mtakatifu kuhusu Sauli na Barnaba. Wakawekea mikono ili kuwaweka wakfu wakatende kazi njema. (13:3).
- Sauli na Barnaba wakatumwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu (13:3,4).

Tambua pia kwamba Roho Mtakatifu aliwaita Sauli na Barnaba, kanisa la mahali (Antiokia) ndilo lililowatuma. Wanachama na viongozi wa kanisa kwa pamoja walithibitisha kukubali kwamba watawategemeza Sauli na Barnaba, waliopelekwa na Mungu kupitia kanisa lao.

Baadaye kanisa liliwakaribisha na kuitisha mkutano maalumu ambapo walisikiliza na kupokea taarifa za huduma yao. Mambo yote aliyofanya Mungu akiwa pamoja nao, na jinsi alivyowafungulia watu Wamataifa mlango wa imani (14:27).

Kanisa lao lilikwa radhi kuongozwa na Roho Mtakatifu. Nao walifurahishwa na kuendelea kuwatuma baadhi ya waumini wao kwenda kumtumikia Mungu ng'ambo ya nchi yao. Waliwaombea na wakatiwa moyo kwa huduma ambayo Mungu aliwapa. Pia walimshukuru Mungu waliposikia kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya wamishionari hao kupitia kuhubiri kwao na huduma ya Yesu Kristo.

**Kwa nini mitume waliwawekea mikono watu vichwani?**

"Kuweka mikono" ni tendo la kuweka wakfu na kubariki, tendo hilo linatajwa mara kadhaa katika kitabu cha Matendo na Waebrania (6:2). Yesu aliwagusa wagonjwa na kuwaponya (Mk 6:5). Paulo (Sauli) aliweka mikono juu ya watu alipokuwa akiwaombea ili waponywe. (28:8-9). Timotheo alipokea karama ya Mungu kwa kuwekewa mikono na Paulo (2 Tim. 1:6). Paulo alipokuwa ameweka mikono yake juu ya wanafunzi kule Efeso, walipokea Roho Mtakatifu wakaanza kunena kwa lugha mpya na kutabiri. Tukio hilo pia lilitokea kule Samaria wakati mitume (Petro na Yohana) walipowawekea mikono waumini, nao wakapokea Roho Mtakatifu (8:17). Viongozi wa kanisa waliomba na kuwawekea mikono viongozi wapya waliochaguliwa kwa kazi maalumu ya ushemasi; wahubiri na waalimu na wamishonari (6:6, 1 Tim. 4:13-14; 13:3).

Paulo alionya kwamba watu wasiitwe na kuwekewa mikono kwa haraka (1 Tim. 5:22). Kuwawekea mikono watu wa Mungu juu ya vichwa vyao ili wapokee baraka maalum chini ya upako wa Mungu ni tendo lililoanza katika Israeli miaka 1700 kabla ya Kristo kuwepo (Mwanzo 48:5-20, Hesabu 8:5-20). Viongozi waliojazwa Roho Mtakatifu tu ndio waliopaswa kuwawekea mikono waumini wengine. Hivyo mtu anayesumbuliwa na mapepo asiweke mikono yake juu ya watu wengine, na wale waliosumbuliwa wasiwekewe mikono.

## HUDUMA YA SAULI NA BARNABA KULE KIPRO

Sauli na Barnaba walimchukua Yohana Marko ili awasaidie (13:5). Wakateremkia Seleukia, kutoka wakasafiri baharini hata kisiwa cha Kipro; mahali alipozaliwa Barnaba.



upepo ulipokuwa umetulia (27:12,13). Hapa palikuwa ni mahali salama kukaa wakati wa baridi.

Meli ikashikwa na tufani kuu, na kuwapeleka mbali na nchi kavu. Mabaharia wakatupa kila kitu baharini ili meli ipunguze uzito na kuiokoa isizame walikaa bila kula chakula kwa siku nyingi na kukata tama ya kuokolewa (27:20).



**Paulo avunjikiwa meli**

Usiku mmoja malaika aliongea na Paulo "Usiogope Paulo, huna budi kusimama mbele ya Kaisari, tena na Mungu atawaokoa watu wote waliosafiri pamoja" (27:24).

Paulo aliwaambia, "changamkeni jipeni moyo, wanaume. Namwamini Mungu yatakuwa vilevile kama nilivyoombiwa" tutaokolewa, lakini lazima tupwelewa katika kisiwa kimoja" (27:25-26).

Baada ya siku 14 katika dhoruba, maji yakapungua (27:27). Wakashusha nanga kuishikilia meli mahali hapo mpaka kuwe kumekucha (27:29). Paulo aliwaambia wale wanaume 276 kwamba hakuna atakayekufa hata mmoja. (27:34,37). Alitwaa mkate akashukuru Mungu na akawapa wale. Walikuwa wamejaa tumaini na kula chakula zaidi kabla ya kutupa mizigo baharini ili kuifanya meli iwe nyepesi (27:35-37. Kulipokucha, waliona pwani yenye mchanga na kujaribu kuipeleka meli huko. Haraka ikawa Kwenye maji hata na kwa sababu ya mawimbi makubwa ikavunjika. Askari wakataka kuwaua wafungwa, lakini yuko aliyewaokoa kwa sababu ya Paulo na imani yake. Ndipo baadaye wakaogelea mpaka ufukweni, wengine wakashikilia vipande vya mbao, kila mtu akafika nchi kavu kwa usalama (27:44). Mungu akawaokoa wote.

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 28

**Jifunze kuhusu:** *Jinsi watu wa Malta walivyookolewa kupitia Paulo (1-10); jinsi waumini wa Italia walivyomkaribisha Paulo (11-16), kusudi la Mungu kwa kanisa la ulimwengu la Yesu Kriso katika siku za maisha ya Paulo (17-30).*

## PAULO KATIKA KISIWA CHA MELITA

Hapo ilikuwa katika nchi ya Malta, watu wa huko walikuwa wakarimu sana (28:2). Wakakoka moto ili watu hawa wapte joto na kukauka. Paulo alipokuwa akiokota kuni, nyoka alimzonga mkononi; labda kwa meno yake.

- Kristo aliye Masihi atateswa (Isa. 53).
- Atafufuka kutoka kwenye kifo (Zab. 16:10).
- Alikuja kuokoa wafu wake, Wayahudi, kwanza (Lk. 1:54-55).
- Wokovu wa Mungu utakuwa kwa ajili ya watu wote (Isa. 42:6, Lk. 2:32).

Karibu mfalme Agripa amwamini Yesu. Akamjaribu Paulo akisema kwamba alikuwa na wazimu (26:24), "wadhani kunifanya mimi mkristo (26:28)? Paulo alipomwambia, "Namwomba Mungu…uwe kama mimi, isipokuwa vifungo hivi (26:32).

Agripa alisimama na kuondoka. Mfalme alisemezana na Festo na watu wengine waliokuwa naye akisema, "kwa sababu gani mtu huyu afe au akafungwe ikiwa hakutenda neno lolote linalostahili kifo wa kungwa? (26:31). Agripa akamwambia Festo, "mtu huyo angeweza kufunguliwa, kama asingalitaka rufaa kwa Kaisafi" (26:32).

Hivyo Paulo akapelekwa Rumi kwa meli, kesi yake ikasikilizwe na Nero, Kaisari wa Himaya ya Rumi.

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Kwa nini Paulo alisema na mfale Agripa (25:13-22)?
2. Kwa jinsi gani Paulo alionyesha kuujua msimamo wa mfalme kuhusu dini ya Kiyahudi (26:3,26-27)?
3. Katika yote aliyoyasema Paulo, yapi ni ushuhuda wake mwenyewe (26:4-21)? Jadili mambo yote aliyosema.
4. Aliunga mkono vipi alichosema na nukuu kutoka Agano la Kale (26:22-23)?
5. Kwa nini mfalme alijaribu kumkatisha tama asiongee naye (26:24,28)?
6. Maombi ya Paulo kwa Festo yalikuwa nini (26:29)? Agripa alionyesha hisia gani (26:30-31)?

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 27

**Jifunze kuhusu:** *Jinsi Mungu alivyowalinda Paulo na wengine waliokuwa melini wakienda Rumi (m. 1-44).*

## MELI YAVUNJIKA PAULO AKIENDA RUMI

Paulo alikuwa kifungoni kwa miaka miwili. Rafiki yake, Aristaiko, aliyemwita mfungwa pamoja naye (Kol. 4:10) na Luka, walikuwepo katika msafara huo.

Yulio, akida wa kikosi cha Augusto, aliwalinda wafungwa wote. 27:1). Akimwamini, Paulo, Yulio alimpa ruhusa aende kuona rafiki zake walioishi kule Sidoni. (27:3).

Kipindi hicho kilikuwa baada ya katikati ya mwezi Septemba, mwanzo wa kipindi cha dhoruba, Paulo akifahamu kuwa ilikuwa ni hatari sana alimwambia nahodha (27:10), lakini mmiliki wa meli hakumsikiliza, hivyo mlinzi naye akapuuzia ushauri wa Paulo. Wakaelekea Foenike katika Kisiwa cha Krete,



Wakaenda kwanza kwenye masinagogi ya Wayahudi, na kuhubiri kuhusu Masihi, Yesu Kristo (13:5).

Liwali wa Kipro aliitwa Sergio Paulo aliyasikiliza mahubiri yao. Alitaka kulisikiliza Neno la Mungu lakini Bar-Yesu, Myahudi aliyekuwa mchawi (jina lingine aliitwa Elima) alijaribu kumzuia liwali asisikie kuhusu Yesu Kristo. Huu ulikuwa upinzani wao wa kwanza. Katika huduma, ingawa walijua kuwa kanisa lao kule Antiokia lilikuwa linawaombea. Hapo ndipo mahali Sauli alitumia jina lake la Kirumi Paulo (13:9). Mara nyingine yatubidi kumpinga shetani na kuchukua mamlaka katika jina la Yesu kwa watu waliopagawa na nguvu za mapepo. Roho Mtakatifu tu ndiye anatuongoza nini tufanye, kama alivyomwongoza Paulo.

Mara baada ya kumwamini Kristo, Paulo alijazwa nguvu za Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono na Anania kule Dameski (9:17). Akijaa Roho Mtakatifu, akamkazia Elima nakumwambia "wewe ni mwana wa ibilisi……. Mkono wa Bwana u juu yako, nawe utakuwa kipofu (13:9-11).

Elima akawa kipofu kwa muda. Ndipo Yule liwali wa kirumi alipoona yale yaliyotendeka kwa Elima, akaamini. Akayastajabia mafundisho ya Paulo kuhusu Bwana Yesu (13:12).

Tunapofundisha na kutii kweli za Mungu, watu wataona tofauti katika maisha yetu.

## PAULO AWAHUBIRI WAYAHUDI NA WAMATAIFA

Walipotoka Kipro, Paulo na rafiki zake walienda mkoa wa Asia wa Himaya ya Rumi. Huko ndiko Yohana Marko alipowaacha lakini hatujui sababu yenyewe. (2 Tim. 4:11). Paulo hakufurahishwa na Marko, ambaye alikuwa mwamini mchanga bado. Kwa hiyo hakuwa na maono yenye nguvu ya kumtumikia Bwana wakati huo. (15:38). Baadaye Paulo alijifunza kuwaamini na kufanya kazi na waumini wachanga, akiwemo Marko.

Wakati Paulo na Barnaba walipotembelea miji mingine, waliyatembelea masinagogi ya Wayahudi ambapo Wayahudi walikutana kusikiliza viongozi wao wakiwasomea maandiko ya Agano la Kale kwa Kiebrania. Wayahudi wa Antiokia ya Pisidia walimwomba Paulo aseme neno la kuwafaa watu, naye alihubiri ujumbe mkuu (13:16-41).

**Masihi au Kristo**

Kusudi la kimbingu la Mungu lilikuwa ni kumtuma Masihi wake, Mwana wake, kwanza kwa wateule wake, Wayahudi. Baada ya maisha, kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo, watu wengi zaidi waliamini kwamba alikuwa Mwana wa Mungu, Wayahudi na watu wa mataifa pia.

Agano la Kale linatuambia kuhusu Masihi aliyeahidiwa. Ilibidi Paulo ayaelewe mambo haya kabla ya kuanza kuhubiri Habari Njema za Yesu Kristo.

Roho Mtakatifu alimpa nguvu na uelewa wa kutenda hayo ili Wayahudi na watu wengine Wamataifa wapokee wokovu wa Mungu kupitia Kristo peke yake. Watu wengi walimwamini Yesu Kristo na kuokolewa. Paulo alianzisha au kupanda makanisa mengi katika himaya ya Kirumi ya wakati ule.

Zituatazo ni unabii 20 ambazo Paulo aliziamini kuhusu Yesu zilizo katika Agano la Kale; zilizotimia wakati wa Paulo: -

1. Yesu ni Masihi aliyeahidiwa (Kristo), Mwana wa Mungu, Mwokozi wetu. (Kumb. 18:15; Yer. 13:5; Isa. 53:12).
2. Yesu ni mponyaji aliyeahidiwa (Isa. 35:5-6).
3. Yusufu aliyemuoa mama yake Yesu alitokana na ukoo wa Ibrahim na ukoo wa Mfalme Daudi. (Isa. 9:7)
4. Mungu aliahidi kuwa kupitia Ibrahimu, mataifa yote ya dunia yatabarikiwa (Mwa. 12:2-3; 18:18).
5. Yesu alizaliwa katika mji wa Bethlehemu, kutokana na familia mkoa wa Yuda. (Mika 5:2).
6. Yesu alizaliwa kama Mwana wa Mungu, na bikra aliyekuwa ameposwa, lakini akaonekana na mimba kabla hajakaribiana na mwanaume (Luka 1:35, Isaya 7:14).
7. Yesu alipokuwa mtoto alipelekwa Misri kwa ajili ya usalama wake (Hosea 11:1).
8. Yesu alikwenda Galilaya kufundisha watu (Isaya 9:1-2).
9. Yesu alikuwa "Nabii Mkuu" aliyezungumziwa na Musa (Kumb. 18:15)
10. Yesu ni Kuhani wetu milele (Zaburi 110:4).
11. Yesu alikuwa na roho ya hekima na ufahamu (Isaya 11:2).
12. Yesu alikataliwa na watu (Isaya 53:3).
13. Watu wengi walimkaribisha Yesu alipoingia Yerusalem kama mfalme mnyenyekevu amepanda mwana punda (Zek. 9:9).
14. Yesu alisalitiwa na mmoja wa wanafuzi wake (Zaburi 41:9).
15. Yesu alisalitiwa kwa vipande 30 vya fedha (Zek. 11:12)
16. Watu wengi walimtolea Yesu ushahidi wa uongo (Zab. 27:12).
17. Yesu hakufunua kinywa chake aliposhtakiwa (Isa. 53:7).
18. Yesu alikufa akihesabiwa pamoja na wakosaji (Isa. 54:12).
19. Mikono na miguu ya Yesu ilitobolewa kwa misumari (Zab. 22:16).
20. Watu walimcheka Yesu na kumdhihaki alipoangikwa msalabani (Zab. 22:6-8).



5. Feliki na mkewe walitumia njia tatu zipi kuonyesha kuwa walikuwa upande wa Paulo (24:24,26,27)? Hali hiyo ilimfanya akawa salama kwa namna gani gerezani?
6. Mpango mpya wa kumuua Paullo ulikuwa upi (25:1-5)? Kwa nini Paulo aliambiwa ilibidi aende kushtakiwa Rumi (25:10-12)?


**Fikiria kuhusu hili:** Soma Marko 13:9-11 na 9:15-16. Unakumbuka kuwaombea Wayahudi wanaoteseka na Wayahudi waliomwamini Kristo, na Pia wakristo wa mataifa wanaoteswa? Tafuta kumweleza Mungu wa Agano la Kale na Agano Jipya katika mafundisho na matukio na umuhimu wake.

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 26

**Jifunze kuhusu:** *Umuhimu wa maelezo ya Luka kuhusu kuokolewa kwa Paulo (1-15); maelezo ya huduma ya Paulo (16-21); maneno ya unabii aliyoyasema Paulo kutoka Agano la Kale (22-23); mwitikio wa Festo na Agripa (24-32).*

## PAULO ANATOA USHUHUDA WAKE KWA MFALME

Siku iliyofuata, mfalme Agripa alikutana na Paulo. Unabii wa Anania kuhusu Paulo katika 9:15 "alichukue Jina lanu mbele ya Mataifa na wafalme na wana Israeli"





**Paulo aliwahubiria wafalme habari za Yesu**

Paulo alimshukuru Mfalme Agripa kwa kumpa nafasi ya kuongea naye kuhusu imani yake na upinzani alioupata (26:2). Pia alimwambia mfalme kuwa alifurahi kwa jinsi alivyoelewa mengi kuhusu dini ya Kiyahudi (26:3).

Paulo alimweleza mfalme kwamba awali yeye hakuamini kuwa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Hivyo aliwaadhibu watu wote waliomfuata Yesu. (26:9-11).

Paulo akazidi kueleza jinsi alivyokutana na Bwana Yesu aliyefufuka akiwa anakwenda Dameski (26:12-18) na jinsi alivyohubiri kuhusu Yesu kwa Wayahudi na Mataifa (29:19-20). Alisema kuwa hiyo ndiyo ilikuwa sababu ya viongozi wa Wayahudi kujaribu kumuua (26:21).

Paulo alifundisha mambo yaleyale ambayo Musa na Manabii walisema, yatatokea (26:23).

**Fikiria kuhusu hili:** Je, unakumbuka kuwaombea Wayahudi ukijumuisha wayahudi waliomwamini Kristo? Utafute kumwelewa Mungu wa Agano la Kale na thamani ya Maandiko hay oleo.

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 25

**Jifunze kuhusu:** *Jinsi Wayahudi walivyotaka kumlagai mtawala mpya wa kirumi aliyeitwa Festo (1-3); Namna Paulo alivyotaka kuwa na amani na Wayahudi (4-9); Kwa nini Paulo aliomba kwenda kushitakiwa Rumi (10-12); Jinsi Festo alivyomtumia Agripa kujua na habari nyingi zaidi kuhusu Paulo (13-27).*

## PAULO ANAOMBA KUONGEA NA MFALME

Baada ya Festo kuwa Gavana alisikia viongozi wa Wayahudi wakisema vibaya dhidi ya Paulo. Wakamwomba Festo atoe amri kwamba Paulo aletwe Yerusalemu kwenye mahakama ya Wayahudi, wapate kumwuua.

Festo hakuwaruhusu hilo, akawataka Wayahudi waende kwenye baraza la Kaisaria. Hivyo wakatoka Yerusalemu kumshitaki Paulo wakaleta mashitaka mengi dhidi yake, lakini hawakuweza kuyathibitisha (25:7).

Mwishoni, Paulo alisema, "Nataka rufani kwa Kaisari". Festo alipokwisha kusema na watu wa baraza akajibu, umekata rufani kwa Kaisari! Basi utakwenda kwa Kaisari (25:12). Kaisari wakati huo alikuwa Nero, aliyekuwa Mkuu wa Himaya ya Rumi; ambaye ilitawala Yudea wakati huo (Baadae Nero aliwatesa Wakristo).

Siku chache baadae, mfalme Agripa II, na dada yake Bernike walifika Kaisaria kumwamkia Festo. Mkuu wa Himaya ya Rumi alikuwa amemteua Agripa awe mfalme wa Wayahudi, Agripa akasema, "mimi nami nalitaka kumsikia Paulo huyo akisema" (25:22). Agripa II alikuwa Kilembwe wa Mfalme Herode Mkuu, aliyetaka kumwua Yesu alipokuwa mtoto (Mathayo 2:16).

Festo alimleta kwa furaha Paulo aulizwe maswali na mfalme Agripa. Festo alisema kwamba alihitaji msaada wa mfalme kumpeleka Paulo kwa Mkuu wa Himaya ya Rumi na orodha ya makosa anayoshtakiwa nayo. "kwa kuwa naona ni jambo lisilo na maana kumpeleka mfungwa, bila kuonyesha mashtaka dhidi yake" (25:26-27).

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Maneno ya Paulo yalisababishaje Masadukayo na Mafarisayo kuhojiana (23:1-8)? Mahojiano hayo yalimsaidiaje Paulo abaki salama kama mfungwa wa Warumi?
2. Ni mambo yapi matatu Mungu aliasema kumtia moyo Paulo (23:11)?
3. Mungu alimtumia nani kumwokoa Paulo na wafanya ghasika (23:12-35)? Paulo aliwekwa vipi salama na Feliki, gavana wa Kirumi?
4. Paulo alieleza njia ya viongozi wa Wayahudi ilivyomletea shida (24:10-21)?



**Watumishi wasafirio (Matendo 13-16)**

Katika Agano Jipya tumeona mifano mingi ya watumishi wa Yesu waliokuwa wajumbe waliotembelea au kuandikia makanisa mengine.

Kama mhubiri na mwinjilisti, Paulo alisafiri kwenda sehemu mbalimbali akihubiri Habari Njema za Yesu Kristo. Alianzisha au kupanda makanisa na kuweka wachungaji.


Baadae Paulo alirudi tena kutembelea yale makanisa, kuwafundisha ukweli za Mungu zaidi na akawatia moyo waifuate njia ya Yesu (14:21-22; 16:4-5). Pia aliandika barua kwa makanisa haya akielekeza kweli za Mungu na mafundisho ya Kristo (15:23). Mtu anayefanya hivyo huitwa mwalimu. Nabii ni mtu anayesema maneno aliyopewa na Roho Mtakatifu, kwa wauumini.

Wahubiri, wainjilisti, na manabii, waalimu wanaotembelea kutoka mji fulani kwenda mji mwingine wanaitwa "watumishi wasafirio" wanaweza kuleta baraka nyingi, kutia moyo na kuleta umoja kwa waumini wake. Watumishi huwa lazima;

- Wawe wanyenyekevu, waliochaguliwa na kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu (13:2).
- Wawe watumishi waliothibishwa na kuteuliwa na viongozi na washirika wa makanisa yao ya nyumbani wanapoishi (13:3).
- Wawe tayari kufanya kazi kwa bidii bila kutegemea malipo kwa kazi hiyo
- Wategemezwe na makanisa yao ya nyumbani yanayowaombea, kuwaongoza na kuwasaidia waendelee kuwa waaminifu.

Miongozo hiyo minne inasaidia kuepukana na watumishi waovu ambao wanasafiri kutoka sehemu fulani kwenda sehemu nyingine bila kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu au kuteuliwa wanapotumika kama wamishionari kwa wasioamini, kama sehemu ya wito wao kutoka kwa Mungu, wanahitaji kutegemezwa kwa maombi.

**Maswali:** Je kanisa lako ni "kanisa Linalowatuma" watumishi? Je kanisa lako hupeleka, kuwategemeza na kuwatia moyo watumishi wasafirio? Je huwa unashiriki kazi ya kuyatia moyo makanisa mapya, huwa mnawaombea wale wanaofanya kazi hii (12:5)? Je, huwa mnawatia moyo au kushiriki katika huduma ya kuwaandikia barua? Je, kanisa lenu ni kanisa la "kupokea wamishionari"? Kanisa huwa linapokea na kuiwakaribisha wainjilisti, wahubiri, manabii na walimu kutoka kwenye makanisa mengine? Mnashirikiana kwa ukaribu na makanisa yanayotuma watumishi? Mnasaidia kulipia gharama zao au kuwapa zawadi?




**The Roman Empire at the time of Paul**

ASIA, GALATIA and PISIDIA were part of Asia Minor, now part of Turkey.

Hivi ndivyo Paulo alivyohubiria umati wa watu akitumia maneno mengi kutoka Agano la Kale.

- Aliwakumbusha watu kwamba Mungu aliwatukuza Wayahudi katika nchi ya Misri, akawavumilia jangwani kwa miaka 40, na kuwaongoza hadi Nchi ya Ahadi ya Kaanani (13:17-20).
- Aliwaeleza kuwa kupitia uzao wa Mfalme Daudi Mungu atawaletea Israel Mwokozi Yesu kama Masihi wao aliyeahidiwa (13:23,32).
- Alihubiri Habari Njema za Masihi wa Mungu kwamba kila atubuye na kumwamini Yesu atasamehewa na kupatanishwa na Mungu kama ilivyoahidiwa awali. Alisema kwamba imani kwa Yesu ni zaidi ya imani kwa Torati ya Musa. Yesu anatoa uzima wa milele kupitia ushindi wake juu ya kifo na dhambi (13:32,38-39). Alimalizia kwa kuwaonya watu wasiudharau ukweli huu. (13:40-41).

Watu wengi wa mataifa waliamini wakafurahi na kujazwa na Roho Mtakatifu (13:48). Baada ya makanisa mapya kuanzishwa, baadhi ya Wayahudi walianzisha ghasia nyingi na kuwasumbua sana Paulo na Barnaba. Waliukataa ukweli wa Mungu na tumaini la uzima wa milele kupitia kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo. (13:46). Hii ni sehemu kubwa ya Habari Njema za wokovu. Wakawatoa mitume nje ya mipaka yao (13:50).

Mahubiri ya Paulo yaliwafaa sana Wamataifa kiasi kwamba baadhi ya Wayahudi waliona husuda (13:42-46). Wakakataa kumwamini Yesu Mwana wa Mungu na wakachagua kuiamini Torati ya Musa. Ufahamu wa Paulo kuhusu makusudi ya Mungu katika Agano la Kale alikataliwa na Wayahudi waliomcha



## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 24

**Jifunze kuhusu:** *Jinsi viongozi wa Kiyahudi walivyomwambia Feliki kuhusu Paulo (mistari 1-9); Paulo alivyosema ukweli kuhusu yeye mwenyewe (10-21); Jinsi Paulo alikuwa na uhuru wa kufundisha na kukutana na marafiki akiwa mfungwa kule Yerusalemu (22-27).*

## PAULO ANAMWELEZA LIWALI WA KIRUMI KWELI YA MUNGU

Baada ya siku tano, baadhi ya Wayahudi kutoka Yerusalemu wakaja Kaisaria kuongea na Felixi. Walimwambia Felixi kwamba Paulo alikuwa amesababisha ghasia nyingi sana kwa Wayahudi duniani kote. Walimweleza kuwa Paulo alikuwa kiongozi wa madhehebu ya "Wanazarayo" (24:5).

Paulo alimwambia Felixi kwamba yeye alikuwa Myahudi mwaminifu na pia mfuasi wa Yesu (24:14). Paulo alikuwa hakufanya kitu chochote kibaya dhidi ya Torati ya Musa. Aliamini kila kitu katika Agano la Kale, na alijaribu kufanya yote yaliyokuwa sahihi machoni pa Mungu na wanadamu. (24:16). Felix alielewa kila kitu alichosema Paulo (24:22) na kuwaondoa Wayahudi:

Felixi akaruhusu rafiki zake Paulo wamtembelee na kumpatia mahitaji yake (24:23). Aletwe amsikilize kuhusu imani yake. Paulo aliishuhudia imani yake kwa Yesu Kristo (24:24). Pia alizungumzia kuhusu:

1. Haki: namna ya kufuata Yesu
2. Utakatifu: namna ya kuwa na maisha bora na kuhusiana na watui wengine tukiwa na maadili safi
3. Hukumu: jinsi atakavyowahukumu watu wote kupitia Yesu.

Felixi aliogopa wakati Paulo alipozugumzia kuhusu haki, utakatifu na hukumu itakayokuja, Felixi aliogopa (24:25). Alitaka Paulo ampe fedha ili amwachie huru (24:26) lakini Paulo alikataa kumpa Felixi rushwa. Badala yake Paulo alimwambia Felixi kweli za Mungu. Kuomba na kutoa rushwa sio njia inayompendeza Mungu.

Baada ya miaka miwili, Porkio Festo akatawala badala ya Felixi. Ili kuwafurahisha Wayahudi alimuacha Paulo kifungoni (24:27).

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Kwa nini Masadukayo walihojiana na Paulo na pia Mafarisayo (23:8)?
2. Mungu alimtia moyo Paulo namna gani (23:11)?
3. Mkuu wa Jeshi la kirumi alisema nini kuhuisu Paulo (23:29)
4. Paulo aliwatorokaje Wayahudi (23:12,16,23,25)?
5. Kwa nini Feliki aliogopa kumsikiliza Paulo (24:25)?

Baadhi ya Wayahud walitaka kumdhuru Paulo. Hivyo mkuu wa Jeshi aliamuru askari wake kumpeleka Paulo kwenye gereza la kijeshi.

**Mambo yanapokwenda vibaya**

Mambo yanapoonekana kwenda vibaya, tunafikiri kuwa Mungu ametuacha. Katika Biblia yote, Mungu mara nyingi alisema moja kwa moja na watu wake. Kabla ya kupaa mbinguni, Yesu alisema, "Nimepewa mamlaka yote" (Mathayo 28:18).

Sharti tukumbuke kwamba Mungu alimpa mamlaka Mwanawe, Bwana Yesu, ya kuamua nini kifanyike mambo yanapoharibika. Kupitia Roho wake, tunamwona Bwana akimwongoza Paulo (Matendo 23:11).

- Yesu aliongea katikati ya usiku
- Yesu alimtokea Paulo akasimama karibu naye.
- Yesu alikuja kumtia moyo
- Yesu alimwambia akamshuhudie pia kule Rumi

Unapopata matatizo, amini kwamba Yesu atakuwa pamoja nawe na atakuongoza. Wakati mwingine yeye atakujulisha yatakayokupata baadaye. Hatuaambii mengi kuhusu wakati ujao, ili tujifunze kuishi kwa imani. Paulo hakujua mengi sana kuhusu wakati utakaofuata baadae, isipokuwa alijua kwamba siku moja atakwenda Rumi (23:11). Mungu hutuonya tusijaribiwe na mawazo yanayovutia au njozi. Kuhusu mambo yajayo, hasa kutoka uchawi, wabashiri wenye kuwasiliana na mizimu au roho za wafu (Kumb. 18:10-13). Anatutaka tumwamini na kutii uongozi wa Roho Mtakatifu aliyeahidiwa kuwa ndani yetu (Yohana 14:25-26).

## FARAJA NA ULINZI WA PAULO

Usiku ule, Bwana Yesu alisimama karibu na Paulo akamwambia "Jipe moyo, uwe hodari, umenishuhudia hapa Yerusalemu, imekupasa kufanya hivyo hivyo Rumi nako" (23:11). Maneno haya yalimfariji na kumtia moyo Paulo, akayakumbuka katika nyakati ngumu zilizofuata baadae.

Wayahudi walipanga kumuua Paulo. Mtoto wa ndugu yake aliposikia haya, akamtembelea gerezani. Paulo akamtuma kijana huyo kwa mkuu wa Jeshi la Kirumi na kumweleza mpango huo wa kuuawa kwake (23:12-22).

Yule mkuu wa Jeshi aliamuru askari wake wamchukue Paulo na kumpeleka Kaisaria wakati wa usiku. Paulo alitaka kumuona Feliki; Liwali wa kirumi wa Yudea, Wilaya kuu ya Israeli (23:24). Huko Paulo atapata kusikilizwa utetezi wake vizuri. Kwa njia hii Mungu alimlinda Paulo na maadui wake.



Mungu kule Antiokia ya Pisidia. Paulo alitamani wampokee Yesu Kristo kama Masihi

Baada ya kuwachagua wazee wenye imani thabiti katika kila Kanisa, Paulo na Barnaba walifunga na kuomba, na kuwaweka katika mikono ya Bwana. Ni muhimu makanisa yapate wazee wa Kanisa wasidie kuongoza, kufundisha na kutunza washirika. Paulo alifahamu kuwa haitoshi kuwa nawahubiri wakiongoza vikundi mbalimbali makanisani.

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Ni vipawa vipi maalumu vilitambuliwa katika kanisa la Antiokia (13:1)?
2. Vipawa hivi viligundulikaje na kutumikaje (13:20-3)? Je, kanisa lako linatoa nafasi ya kumsikiliza Mungu?, Je, kanisa lako huwa linawatuma wahubiri wamishenari kwenda nje?
3. Ni kitu gani kilimsababisha Liwali wa Kirumi kumwamini Bwana Yesu Kristo (13:12)?
4. Kwa nini Paulo alisimulia tena historia ya Israeli (13:17-23)?
5. Paulo alisema nini kuhusu kifo na kufufuka kwa Yesu (13:23-31)?.
6. Kwa nini Paulo alinukuu mistari kutoka kwenye manabii wa Agano la Kale (13:32-41)?
7. Wayahudi na Wamataifa mengine waliyapokeaje mahubiri kuhusu Yesu (13:42-52)?

**Fikiria kuhusu hili:** Elezea kazi, ibada, ushuhuda wa Kanisa la kwanza huko Antiokia (13:1-5). Eleza Namna kuhubiri ya Paulo katika pisidia, Antiokia (13:14-41). Je mahubiri ya injili ya Yesu Kristo siku za leo yana matokeo gani?

**Maana ya Kanisa**

Neno "Kanisa"linamaanisha "wakristo wote walioamini, popote walipo ulimwenguni", ambao ni mali ya Bwana Yesu Kristo. Mara nyingi tunawaita waaminio "mwili wa Kristo". Paulo alilielezea Kanisa kama "nyumba ya Mungu aliye Hai, nguzo na msingi wa kweli (1 Tim. 3:15).

Pia kila kundi la mahali tunaliita kusanyiko au ushirika wa waumini". Leo neno 'Kanisa' linatumika kumaanisha majengo ambapo waumini wa mahali hukutana kufanya ibada. Hatuhitaji jengo ili tupate kumwabudu Mungu.

Wakristo wa karne ya kwanza walikutana katika nyumba na mabaraza ya masinagogi ya Wayahudi kila siku ya Sabato (Jumamosi). Palikuwa mahali maarufu kwa waumini kukutana ili wasikilize mafundisho kutoka kwenye Agano la Kale na maneno ya Yesu kutoka kwa mitume.

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 14

**Jifunze kuhusu:** *Kuhubiri kwa nguvu za Roho Mtakatifu kule Ikonia (1-6); kuhubiri na kuponya kule Listra (7-21); jinsi Paulo na Barnaba walivyoyaimarisha makanisa mapya (22-23); kurudi kwenye kanisa lililowatuma la Antiokia ya Syria (24-28).*

### MIUJIZA NA MATESO

Paulo na Barnaba walihubiri kwa uweza mkuu katika mji wa Ikonia. Matokeo yake idadi kubwa ya Wayahudi na Wamataifa waliamini. Hata hivyo kulijitokeza Wayahudi ambao hawakulipenda jambo hilo, wakachochea vurugu dhidi ya Wamataifa walioamini; na kusababisha watu kugawanyika. Kuhubiri Habari Njema za Yesu mara nyingi huwagawa marafiki na hata wanafamilia. Baadhi yao huamini na kuwaacha wengine hawaamini (Mathayo 10:21-23). Watu wengine huogopa kumfuata Yesu,

Paulo na Barnaba walikaa huko muda mrefu (14:3), kwa vile hawakuchoka katika kutenda mema (Gal. 6:9), kukawa na waumini wengi katika mji ule. Habari Njema za Yesu ziliyabadilisha maisha yao. Baada ya kusikia mpango wa kutaka kuwaua, mitume hao wawili waliondoka (14:6) na kuwaaacha waamini walioimarika katika imani kwa Mungu na Mwana wake, Mwokozi wao.

Paulo na Barnaba wakasafiri kwenda Listra na Derbe, wakahubiri kwa ujasiri na Mungu akawajalia ishara na maajabu yaliyotendeka kwa mikono yao. Kule Listra watu walipomwona mtu ameponywa, walisisimka. Kwa vile walikuwa wanaamini katika miungu na roho za kipagani, walimwita Paulo "Herme" na Barnaba "Zeu"; majina ya miungu ya Kiyunani (14:12), kwa maana lilikuwepo hekalu la Zeu katika mji huo. Kuhani wa Zeu akataka kutoa dhabihu ya wanyama kwa Paulo na Barnaba. Lakini Paulo alimzuia asifanye hivyo.

Akawaambia watu "sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi ….mgeuke na kuyaacha mambo haya ya ubatili na badala yake kumwelekea Mungu aliye hai (14:15). Ndipo Wayahudi kutoka Antiokia ya Pisidia wakawakasirisha watu na kuwashawishi hata wakampiga Paulo kwa mawe. Wakamburuta nje ya mji wakidhani kuwa amekwisha kufa, lakini kumbe Mungu aliuokoa uhai wake.

### MJADALA KUPITIA MAHUBIRI YA HABARI NJEMA

Siku ya pili yake Paulo na Barnaba waliondoka kwenda Derbe (14:20); walipohubiri na kupata wanafunzi wengi ambao waliamini Habari Njema za Yesu Kristo (14:21).

Baadae Paulo na Barnaba wakarejea katika mji walikopanda makanisa (Listra, Ikonia na Antiokia-ya-Pisidia) wakawatia moyo waumi wapya (14:22-23) kwa: -

- Kuwaimarisha katika imani
- Kuwafundisha wakae katika imani na kweli ya Mungu



- Alipata ruhusa ya kuwafunga wafuasi wa Yesu gerezani na kwaua (22:4-5).
- Alikutana na Yesu akiwa njiani kwenda Dameski (22:6-11)
- Mungu alimtuma mwamini mmoja Myahudi aongee na Paulo, aliyemwambia ashuhudie kuhusu Yesu (22:12-16)
- Kule Yerusalemu Yesu alimtuma Paulo aende mbali kwa mataifa mengine wa watu wasiokuwa Wayahudi. (22:17-21)

Watu waliokuwa wanamsikiliza Paulo aliposema hayo, walitaka kumwuua (22:22). Yule Mkuu wa majeshi aliamuru achapwe viboko (22:29). Lakini mkuu wa majeshi alipogundua kuwa Paulo alikuwa mrumi na myahudi pia akaamuru waache kumchapa. Mkuu wa majeshi alimpeleka kwenye Baraza la Wayahudi, ili ashitakiwe, apate kusikilizwa atakapojitetea (22:30).

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Paulo alielezaje matendo yake kwa watu wenye hasira (22:1-21,)?
2. Je, Roho Mtakatifu alimwongozaje Paulo ili asichapwe viboko (22:22-29)?
3. Yule Mkuu wa Jeshi la Kirumi alifanya nini ili kumpa nafasi Paulo ashitakiwe apate kujitetea mbele ya Wayahudi (22:30)?

**Fikiria kuhusu hili:** Je, we unao ushuhuda binafsi? Unaweza kusema kwa ujasiri mbele ya watu wenye hasira au watu wasioamini kama vile alivyofanya Paulo, kwa ghrama yeyote? Fikiria jinsi Mungu alivyomwokoa Paulo na madhara wakati alipothibitisha kuhusu mambo Mungu aliyokuwa ameyafanya katika maisha yake kama mfuasi wa Yesu.

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 23

**Jifunze kuhusu:** *Jinsi viongozi wa Wayahudi walimtendea nini Paulo (1-4); jinsi viongozi wa dini walivyoshindwa wenyewe (5-10); kusudi la Mungu kwa Paulo (11); kusudi la Wayahudi kwa Paulo (12-13); mambo ambayo mpwa wa Paulo alifanya (14-22); ya kusudi la waamini kwa Paulo (23-35).*

### PAULO ANASEMA UKWELI WA MUNGU KWENYE BARAZA LA WAYAHUDI

Kesho yake, Paulo aliruhusiwa kusema mbele ya Baraza ambalo ilikuwa ni mahakama ya juu kabisa ya Kiyahudi. Alizungumzia tumaini la ufufuo wa wafu. Masadukayo walisema hakuna ufufuo, hivyo walibishana na Mafarisayo, waliamini katika ufufuo wa wafu.

Paulo aliliambia Baraza kwamba yeye alikuwa Farisayo aliyeamini katika ufufuo wa wafu, na katika ufufuo wa Yesu Kristo (23:6). Hili jambo lilisababisha mabishano kati ya viongozi wa kidini. Watu wanaokataa kuamini kweli za Mungu zote mara nyingi huishia kutokubaliana na kubishana wao kwa wao.

**Fikiria kuhusu hili:** Paulo alisumbuliwa na baadhi ya viongozi wa Wayahudi alipowahubiria Wayahudi kuhusu Kristo. Pia Paulo alipata matatizo kutoka kwa Wayahudi waliaoamini kwa vile aliwahubira Kristo watu wa mataifa. Kama ndiyo, kwa nini Roho Mtakatifu alimpeleka Paulo Yerusalemu? Wakati wote muombe Mungu akuonyeshe picha yake kubwa au kusudi lake, unapopitia shida.

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 22

**Jifunze kuhusu:** *Ushuhuda binafsi wa Paulo (1-21); mioyo migumu ya watu walioshika dini (22-23); jinsi watawala wa kirumi walivyomtendea Paulo (24-30).*

## PAULO ANASEMA UKWELI WA MUNGU KWA HALAIKI

Paulo alipokamatwa, aliruhusiwa kusema mbele ya watu. Kwa kiaramu ili wote waweze kumwelewa. Akawaambia: -

- Yeye alikuwa Myahudi aliyeijua Torati ya Musa vizuri sana (22:3)

### Ufufuo wa mwili

Somo muhimu katika kitabu cha Matendo ni ufufuo wa mwili. Paulo aliwaandikia waumini wa Korintho: "Kama hakuna kiyama ya wafu, Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, basi kuhubiri kwetu ni bure. Imani yenu ni bure (1 Wakoritho 15:13-14). Ufufuo wa Yesu Kristo ulikuwa ni muhimu sana kiasi kwamba ulifundishwa katika kila hotuba katika kitabu cha Matendo (1:22; 2:31; 4:2,33; 17:18,32; 23:6; 24:21).

Masadukayo walikuwa ni watu wa daraja la juu la Wayahudi kimaisha (matajiri). Walipinga mafundisho ya Habari Njema za Wokovu kupitia Yesu. Hawakuamini kwamba Yesu Kristo alifufuka kutika wafu wala hawakuamini juu ya ufufuo wenyewe Yesu aliomwahidi kila mwamini.

Agano la Kale linazungumza kidogo tu kuhusu ufufuo. Labda rejeo bora zaidi liko katika kitabu cha Daniel 12:1-2 "Wakati huo … watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu cha uhai (uzima). Tena wengi wa hao waliolala katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele. Wengine wataamka wapate aibu na kudharauliwa milele". Angalio pia 24:15.

Ahadi ya "Uzima wa milele" imetajwa mara moja tu katika Agano la Kale, lakini Wakristo wa Agano Jipya waliamini kuwepo maisha baada ya ufufuo kutoka kwa wafu. Uzima wa milele sio mwendelezo wa maisha yetu ya zamani duniani ila ni maisha mapya pamoja na Mungu mwenyewe (Yohana 11:25; 2 Wakoritho 4:14; 1 Wathesalonike 4:16).



- Kuwaonya wategemee kupata mateso
- Kuwachagulia wazee (viongozi) wa kanisa
- Kuwaombea kwa Mungu awalinde

Paulo na Barnaba walijifunza kumwamini Mungu kwa kazi aliyoianzisha.

Baada ya safari ndefu Paulo na Barnaba walirudi kwenye kanisa lao la nyumbani Antiokia ya Syria, na kuwaelezea mambo yote aliyoyafanya Mungu pamoja nao (14:27).

Mungu aliwatumia Paulo na Barnaba kupanda makanisa. Maombi ya kanisa mama (lililowatuma) kule Antiokia yalikuwa yamejibiwa. Kulikuwepo miujiza ya uponyaji na ukombozi kutoka kwenye mateso, ambapo watu wengi wa mataifa waliokolewa. Waumini wa kanisa la Antiokia walikuwa ni sehemu ya kusudi la Mungu kuufikia ulimwengu.

Paulo na Barnaba waliishi huko pamoja na wanafunzi kwa muda mrefu. (14:28). Kukawa na kazi nyingine alizozifanya katka kanisa.

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Paulo na Barnaba walifanya nini walipoteswa (14:6,20)?
2. Waumini wapya watiwe moyo kwa jinsi gani (14:22)?
3. Je kanisa lako huwa linakuambia Mungu anafanya mambo gani katika maisha ya watenda kazi wengine (14:27)?

**Fikiria kuhusu hili:** Kwa nini ilikuwa muhimu kuyatembelea makanisa mapya (14:21-23)? Kwa nini ilikuwa muhimu Paulo arudi kwenye kanisa lake la Antiokia ya Syria (14:26-28)

### Serikali ya kanisa

Masinagogi ya Wayahudi yalikuwa na kiongozi aliyekuwa ni mwalimu Paulo alifuata utaratibu huo huo alipoanzisha ushirika wa kikristo wa mwanzo. Mashemasi wanawake na wanaume ambao walifundisha na kuwasaidia waumini. Pia kule Yerusalemu kulikiwepo wazee wa kanisa (15:2). Yakobo alikuwa kiongozi (Mzee) wa kundi la Yerusalemu au baraza la makanisa (15:13).

Paulo na Barnaba walirudi kwenye miji ambako walihubiri, wakawatia moyo waumini wapya na kuwachagulia wazee wa kanisa (14:21-23). Baada ya kufanya hayo Paulo na Barnaba walirudi kwenye kanisa lao la nyumbani. Ilikuwa ni muhimu kutoa taarifa kwa viongozi wa kanisa lao waliowatuma kwa mamlaka ya Roho Mtakatifu (13:3)

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 15

**Jifunze kuhusu:** *Jinsi ya kushughulikia matatizo ndani ya kanisa la mahali (1-2); namna ya kushughulikia matatizo kati ya viongozi wa kanisa*

*(10-19); jinsi ya kuleta umoja na mafundisho sahihi ndani ya makanisa (30-35); kwa nini Paulo alikataa kufanya kazi pamoja na Barnaba (36-41).*

## MKUTANO WA VIONGOZI WA KANISA KULE YERUSALEMU

Wakashuka watu waliotoka uyahudi na kuanza kuwafundisha ndugu wa Kanisa la Antiokia wakisema"msipotahiriwa…..hamuwezi kuokoka" (15:1). Tohara ilikuwa ni desturi ya Kiyahudi ya kuondoa govi la uume wakati mtoto alipofikisha siku 8 baada ya kuzaliwa. Mungu alimwamuru Ibrahimu kila mtoto mwanamume wa familia yake atahiriwe, kama ishara ya Agano Lake (Mungu) na Wayahudi (Mwanzo 17:11).

Paulo alikuwa amewafundisha kwamba imani peke yake ilitosha kuwaokoa watu. Hivyo kukatokea mabishano kati ya wauminmi Wayahudi na waumini Wamataifa kuhusu hitaji la kutimiza kanuni ya tohara. Kutokana na kutokukubaliana huko, Wazee wa kanisa la Antiokia wakaamua kuwasafirisha Paulo na Barnaba kwenda Yerusalemu; Tito pia alikwenda pamoja nao (Gal. 2:1). Lengo ilikuwa kwenda kuwauliza Petro, Yakobo na Wazee wa kanisa ili wajue wafanye nini kwa habari ya swala la tohara. (15:2).

Wakiwa njiani walizungumza na Wayahudi waliomwamini Yesu Kristo. Ndugu hao walifurahi sana waliposikia kwamba mataifa nao waliskia Habari Njema za Yesu Kristo. (15:3). Lakini kule Yerusalemu baadhi ya waumimi ambao walikuwa Mafarisayo, hawakufurahishwa, wao walitaka kutunza taratibu za zamani za kidini, pamoja na tohara.

Yakobo na mitume waliwakaribisha Paulo na wenzake kule Yerusalemu. Baadaye Mafarisayo kati yao wakasimama wakawaambia waumini kuwa ni lazima kutii tohara ya Musa na kutahiriwa (15:5). Petro aliwajibu kama hivi "Mungu ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia akiwapa Roho Mtakatifu vilevile kama alivyotupa sisi; wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, akiwapa Roho Mtakatifu kama sisi…akiwasafisha mioyo yao kwa imani (15:8). Petro alisisitiza kwamba ni kwa kupitia neema ya Bwana Yesu tu, kwamba tunaokolewa, vile vile kama wao (15:11).

Basi viongozi wa kanisa wakanyamaza, na wakawasikiliza Paulo na Barnaba. Walizungumzia habari za ishara na maajabu ambayo Mungu aliyafanya kati ya Wamataifa wasiotahiriwa katika miji ya mkoa wa Asia.

Baadaye Paulo aliandika "kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani kwa Kristo (Efe. 2:8)". Wokovu ni karama ya Mungu uzima wa milele katika Kristo Yesu (Rum. 6:23). Dini nyingi za uongo zinasema lazima kufanya kazi fulani kwa bidii na kutii sheria za dini ili uende mbinguni. Paulo alisema wokovu wenu ni kipawa cha Mungu", wala si kwa matendo…bali kwa damu ya Yesu Kristo (Efe. 2:8-13). Kwanza tunaokolewa, na baadaye tutende matendo mema kutokana na imani.



walijitahidi kumfuata Kristo na pia kuifuata Torati ya Musa wakati uleule. (21:20). Kwa sababu hiyo, Paulo aliombwa kuthibitisha kuwa aliiamini Torati ya Musa (21:23-34). Alitaka kuwapendeza watu na kumpendeza Mungu. Lakini muda kitambo Paulo akapata shida kutoka kwa Wayahudi waliokuwa wametoka katika mkoa wa Asia (21:27).

Ndipo akaomba kueleza ukweli (21:39). Maelezo hayo yalichochea ghasia zaidi kutoka kwa Wayahudi wa Yerusalemu (22:22). Petro, hata hivyo, alimsifu Paulo kwa hekima aliyopewa na Mungu na akawaonya wasomaji wake wasimwelewe Paulo vibaya au kupotosha yale aliyosema (2 Pt. 3:15-16).

**Zungumza kuhusu hili.**

1. Jadilianeni kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu katika safari ya Paulo kwenda Yerusalemu (19:6,20:22-23; 21:4,11-13)
2. Waamini walimpa Paulo ushauri gani? (21:4,12)?
3. Waumini walimtia moyo Paulo kwa namna gani (21:14)?
4. Maneno ya Roho Mtakatifu katika 21:11. Yalianzaje kutimia (21:30-40)?

**Mafarisayo na masadukayo**

Mafarisayo na Masadukayo yalikuwa ni makundi mawili ya kidini ya Wayahudi. Yesu aliwaonya waumini wasizifuate njia zao. (Mathayo 16:6; 23:2-3).

Kulikuwepo **Mafarisayo** kadha wa kadha wakati wa Yesu na Paulo, Mafarisayo walikuwa wayahudi wenye kumcha Mungu walioitii Torati ya Musa na sheria za Hekalu. Waliamini katika kweli za Mungu zilivyoandikwa kwenye Agano la Kale, wakijifikiria kuwa wao walikuwa wabobezi wa kuelewa na kuutumia kweli ya Mungu. Waliwaambia watu wafanye nini, waamini nini, na nini wasifanye.



Walijifanyia sheria nyingi. Kwa hiyo, ilikuwa vigumu kwa watu kutii kanuni zao zote na pia wakawa na amani na Mungu. Yesu alisema kwamba mafarisayo wenyewe hawakutii sheria zao wenyewe. (Mathayo 23:3). Na alijua kuwa hakuna hata mtu mmoja angepata amani na Mungu kwa kufuata sheria zilizotungwa na wanadamu.

**Masadukayo** walikuwa Wayahudi matajiri waliotii torati ya Musa lakini hawakujifanyia sheria yoyote mpya. Walisema kwamba watu walitakiwa kuitii Torati lakini wao waamue mambo gani wafanye siku baada ya siku. Walitii desturi za kidini za zamani, ila hawakutafuta uongozi wa Mungu kutoka kwenye neno lake lililoandikwa. Hii ndo sababu iliyowafanya Masadukayo kuhojiana na Mafarisayo kuhusu kutii Torati. Masadukayo pia walikataa kuamini malaika, roho na maisha baada ya kifo (ufufuo wa mwili).

Waumini walijua hatari zilizokuwa mbele, lakini hata hivyo, baadhi yao walikwenda Yerusalemu pamoja na Paulo. Mnasoni, mwenyeji wa Kipro na mwanafunzi wa zamani aliishi katika mji wa Yerusalemu. Maelfu ya watu walikuwakoYerusalemu kwa ajili ya siku kuu ya Pentekoste. Walijaza kila nyumba, lakini Mungu aliandaa mahali maalum kwa ajili ya mtumishi wake, Paulo na rafiki zake, mnasomi (21:16).

Kesho yake Paulo akaenda kuwaona Yakobo na wazee wa kanisa la Yerusalemu (21:17-18). Katika Ugiriki na mkoa wa kirumi wa Asia maelfu watu wa mataifa walioamini. Paulo alitaka kuwafahamisha wazee wa kanisa mambo aliyotenda Mungu kati ya watu wa mataifa kwa njia ya utumishi wake.

Ingawa wazee walimtukuza Mungu, lakini walimwambia Paulo kwamba "kuna Wayahudi wengi [wanaoamini, KJV] wanaojitahidi kushika kwa bidii torati ya Musa.wamesikia kwamba unawafundisha wayahudi kuiacha torati ya Musa. Wanafikiri unawafundisha wasiwatahiri watoto wao na wasiishi wakifuata desturi na mila zetu (Wayahudi). Lazima watasikia kuwa umekuja, hivyo fanya kama tunavyokushauri" (21:20-23).

Walimwambia Paulo achukue hekaluni watu wane aliokuwa nao watakaswe; vichwa vyao kunyolewa na kuwagharamia sadaka zao za nadhri ili kutii torati ya Musa.

Paulo alikubali kufanya hivyo; ingawa yeye wakati wote alihubiri kwa watu waliokolewa kwa neema ya Mungu kwa njia ya imani kwa Yesu peke yake (Efeso 2:8-9). Baadaye waumini huweza kutunza sheria kupitia Roho Mtakatifu ambaye Yesu hutujaza baada ya kuokolewa.

## PAULO ANASHAMBULIWA NA KUKAMATWA

Paulo alitunza Torati ya Musa hapo awali, Alinyoa kichwa chake huko Kenkrea, kwa sababu alikuwa ameweka nadhiri kwa Bwana (18:18)

"Baadhi ya Wayahudi walitoka katika Mkoa wa Asia walimwona Paulo Hekaluni. Walimchukia Paulo wakataka kumuua. Walipiga kelele, "Amemwingiza mtu asiyekuwa Myahudi Hekaluni na kupatia unajisi mahali patakatifu (21:28).

Umati ulipojaribu kumuua Paulo aliokolewa na mkuu wa Jeshi la Kirumi. Baadae Mkuu huyo wa Jeshi alimwendea Paulo, akamtia nguvu na kumwamuru askari wamfunge minyonyoro na kumpeleka ndani ya ngome ya kirumi (21:34-35). Paulo akisimama kwenye ngazi, akaomba kuongea na watu (21:39).

Paulo akahubiri kwamba torati ya Musa ilikuwa njema lakini haiwezi kuokoa watu kutoka kwenye dhambi zao (Warumi 3:20). Alihubiri kwamba watu hupatanishwa na Mungu kupitia Imani katika Yesu Kristo (Warumi 3:22). Alikiri kujua kwamba Torati ilikuwa Kiongozi wa kutuambia kitu gani ni kosa, huonyesha ni nini kilichosahihi na kipi si sahihi.

Kwa wengi, haikuwa rahisi kuelewa. Ndio maana Paulo akapata taabu na baadhi ya Wayahudi walioamini kule Yerusalemu (21:21). Waumini wengi



Yakobo akajibu, "maneno ya manabii yanakubaliana na hiki (15:15). Akitumia maneno ya Nabii Amosi ambaye alizungumzia wakati ambapo Mungu atayabariki mataifa yote kupitia Yesu Kristo.

Hii inamaanisha kwamba watu wote ambao si Wayahudi watakaokuwa mali yangu, na pia mabaki ya Wayahudi wanaomwamini Kristo (15:17, Amosi 9:12). Yakobo akawaonya viongozi wa kanisa "wasiwataabishe wale wanaomgeukia Mungu katika Wamataifa (19). Pia akaonya mitume kuwakumbuka kutunza maskini (Gal. 2:10).

Viongozi wa Kanisa la Yerusalemu wakaandika barua kwa waumini wa mataifa kule Antiokia ya Syria. Wakampa Yuda na Sila wafuatane na Paulo na Barnaba. (15:22-23).

Wawili walikuwa ni wazee (viongozi) wa kanisa la Antiokia. Katika barua ile viongozi wa Kanisa la Yerusalemu, waliomba msamaha kwa vile baadhi ya Wayahudi waliowasumbua walikuwa ni waumini wa Kanisa lao; wasiokuwa Wayahudi huko. Barua hii ilileta umoja kati ya waumini (Yoh. 17:26). Ujumbe wao upo katika barua (15:24-29): -

- Ulitambua tatizo lililokuwepo
- Uliomba msamaha kwa usumbufu uliojitokeza

**Matatizo ya kanisa na mikutano ya kanisa (Matendo 15:1-35)**

Baadhi ya viongozi wa Kanisa walitaka waumini wapya wapate imani kupitia sheria za Musa (15:1). Sheria hizo zilijumuisha kutahiriwa. Wengine walisema kuwa imani kwa Bwana Yesu Kristo iliwaacha huru kutoka kwenye dhambi zao (15:11). Viongozi wa kanisa walikutana na iliwachukua muda wakijadiliana ni kipi kilikuwa sahihi na nini kilikuwa kosa!

- Kwanza kanisa lote lilikutana kushirikishwa mambo yaliyotokea (m. 4)
- Baadaye viongozi wa kanisa walikutana kujadiliana kuhusu matatizo hayo (m. 6)
- Kila mmoja alinyamaza na kusikiliza kwa makini (m. 12)
- Paulo na Barnaba walitoa taarifa kwa kanisa kuhusu mambo ambayo Mungu aliyafanya (m. 12)
- Walisoma kweli za Mungu kwenye Agano la Kale (m. 16-17).
- Ndipo Yakobo, kiongozi wao, alitoa maelekezo kuhusu nini kifanyike (m. 19-21).
- Kanisa lote lilikubali kufuata maelekezo hayo (m. 22).
- Mwisho wakayaambia makanisa mengine juu ya makubaliano (m. 23-29)

Makubaliano hayo yalijumuisha pia wajiepushe kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa miungu, kunywa damu na kula nyama zilizosongolewa na damu. Pia waliyaonya makanisa "wajiepushe na uasherati" (15:29).

- Ulithibitisha jinsi walivyoamini na kufundishwa na Paulo na Barnaba ilikuwa sahihi kabisa.
- Waliwajulisha kile Roho Mtakatifu alichosema na Kanisa kule Yerusalemu
- Uliwaonya wajiepushe kula vitu vilivyotolewa sadaka kwenye ibada za shetani na sanamu, hata nyama ya mnyama aliyekufa kibudu
- Ulitoa ushauri mwingine wa kiroho na kimaadili.

Yuda na Sila walikaa Antiokia mpaka amani iliporejeshwa.

Kama Yakobo lazima tutoe jibu na kuwa sehemu ya maombi ya Yesu kuhusu umoja wa kanisa (Yoh. 17:17). Yaani, kati ya waamini wapya na wale wa zamani, waumini wenye tamaduni tofauti na waumini wapya wa wale wa asili. Hiki lazima kifanyike kwa upendo kama inavyoonekana leo kupitia makusudi ya Mungu katika Agano la Kale na Agano Jipya.

## KUKUA KWA KAZI YA UMISHENI YA PAULO

Mara baada ya hayo Pulo alitaka kurudi kuyaangalia makanisa mapya ya Kipro na Asia. Barnaba alikubali lakini alitaka kumchukua Marko binamu yake Marko aliyekuwa kijanaaende pamoja nao. (15:37).

Paulo hakuona vema kumchukua Marko aende nao. Basi Pulo akaenda na So; a mpaka Asiana Barnaba akaenda na Marko mpaka Kipro. Kutokubaliana huko kulisababishwa na Paulo alipokataa kumwamini mwongofu mchanga aliyekuwa amewacha huko Pamfilia, na kurjee Yerusalemu (13:13). Marko alikuwa binamu yake Barnaba (Kol. 4:10) ndio maana alimwamini. Hata hivyo, Paulo na Barnaba hawakuafikiana.

Tunajua kidogos sana kuhusu barnaba, lakini Marko baadaye alifanya kazi na Paulo Filemoni 24). Marko pia alioandika kitabu cha Injili kujusu mafundisho na huduma ya Yesu.

Kuelekea mwishoni mwa maisha yake, Paulo alimwambia Marko amsaidie (2 Tim. 4:11).

Wakati viongozi wa Kikristo wanapotofautiana ni vizuri watengane, ili kanisa lisigawanyike. Pauloa na Barnaba hawakuwagawa waongofu bali wao wenyewe walienda kila mmoja upande wake, wakaendelea kuhubiri na kufundisha Habari Njema.

Mungu aliwatumia wote kupanda makanisa mapya. Ukweli wa Mungu kuhusu Yesu ulizidi kurnra mpaka mbali sana wakitumia barabara nzuri na meli zilizotyengenezwa naWarumi.

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Kwa nini kanisa lilituma viongozi kwenda Yerusalemu (15:1-2)?
2. Unawakaribisha watu kutoka nje ya kianisa lako ambao wameokoka, na hata waongofu wapya (15:3)?
3. Je kanisa la kwanza lilitatuaje matatizo (15:4-22)?



kanisa wakalia sana, wakamkumbatia na kumbusu (20:37). Paulo aliwaambia kuwa hatawaona tena.

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Utafanyaje wakati maisha yako yapo hatarini kutokana na watu wanaoleta ghasia (20:23, Mt. 2:14-23)? Ililiathiri vipi kanisa lililomtuma Paulo la Antiokia aliposhindwa kurudi?
2. Paulo alifaidika vipi na msaada wa waumini (20:1,4)?
3. Nguvu ya Roho Mtakatifu ilidhihirishwa vipi kupitia Paulo (20:10)? Hii iliwatiaje moyo wa waumini (20:12)?
4. Kwa nini Paulo alitumia muda mrefu akifundisha na kuhubiri (20:7,11,25-31)?
5. Paulo alifundisha nini ili viongozi wa kanisa wawe imara (20:27-28)? Kwa nini ilikuwa muhimu kwa viongozi wa kanisa kufundisha mambo haya (20:29-31)?
6. Paulo aliijenga vipi imani ya waumini wote (20:32,36)?

**Fikiria kuhusu hili:** Unapokuwa na shughuli nyingi katika kumtumikia Mungu, je, huwa unatenga muda wa kumsikiliza Roho Mtakatifu anachokuambia? Je, unazungumza na kuwasikiliza, na kuwatia moyo wale wanaokuombea?

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 21

**Jifunze kuhusu:** *Safari ya Paulo kwenda Yerusalemu (1-16); Paulo alivyotokea Yerusalemu (17-30); Ni kwa jinsi gani watawala wa kirumi waliyaathiri maisha ya Paulo wakati huo (31-40).*

## PAULO ANARUDI YERUSALEMU

Paulo alisafiri kwa meli kutoka Mileto, karibu na Efeso mpaka Tiro (21:1-6). Huko aliwakuta waumini Wakristo waliomwambia kile Roho Mtakatifu alichosema kuhusu taabu atakayoipata Yerusalemu. Lakini Paulo aliamini kwamba Roho Mtakatifu alimtaka aende huko.

Mashua ilipowasili Kaisaria Paulo alikaa pamoja mwinjilisti Filipo. Wakati akiwa huko, Agabo alikuja kutoka Yerusalemu. Alichukua mshipi wa Paulo akajifunga mikono na miguu yake kama ishara. Kisha akasema maneno ambayo Roho Mtakatifu alimwambia, akisema, "Hivi ndivyo wayahudi watakavyomfunga mwenye mshipi huu", (21:11). Paulo, kama Yesu, akajua yatakayompata Yerusalemu.

Paulo akawajibu Agabo na waumini "kwa nini mnatoa machozi? Niko tayari, sio kufungwa tu, hata kufa kule Yerusalemu kwa ajili ya jina lake Bwana Yesu (21:13).

Paulo alizuiliwa kurudi kwenye kanisa lake la nyumbani kule Antiokia. Alisikia kwamba viongozi wa Wayahudi walitaka kumkamata. (20:3). Badala yake alisafiri kupitia Makedonia mpaka kwenye mkoa wa Kirumi wa Asia, akatweka mpaka kupitia Efeso. Paulo hakuweza kuiona nchi ya Ugiriki au Syria tena, na hata kanisa lake la nyumbani.

Ndugu saba katika Kristo walienda naye mpaka Makedonia, wakatangulia Troa na kumsubiria huko. Akaungana nao huko na kukaa pamoja nao kwa siku saba. Waumini walikutana katika ghorofa na Paulo akaongea nao mpaka saa sita usiku. Kulikuwepo na joto, chumba kikiwa kimejaa moshi uliotoka kwenye taa za mafuta. Kijana mmoja aliketi dirishani, akazidiwa na usingizi sana hata akaanguka mpaka chini na kufariki. Paulo akashuka akamwangukia, akamkumbatia, na roho yake ikamrudia (20:10).

Baada ya muujiza huu, Paulo akapanda tena ghorofani akala chakula, akaendelea kuwafundisha watu mpaka alfajiri pamoja kuumega mkate na meza ya Bwana kama Yesu alivyowaagiza wanafunzi wake katika karamu ya Mwisho (20:11; 14:19; Lk. 22:19).

Ndipo akaenda zake kwa merikebu hadi Mileto. Kwa njia hii aliokoa muda katika safari yake kwenda Yerusalemu**.**

## PAULO ANAONGEA HARAKA NA VIONGOZI WA KANISA

Akiwa Mileto, Paulo akawatuma watu kwenda Efeso kuwaita wazee wa kanisa. Akawaambia maneno mazito akisema "Ninyi wenyewe mnajua ya kuwa sikumruhusu mtu awaye yeyote kunizuia kuwahubiri ninyi. Nimwaeleza wote wayahudi na wayunani(mataifa) kwamba lazima wamgeukie Mungu na kugeuka kuziacha dhambi zao. Kwamba lazima kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo"(20:19). Hakuwahi kushindwa kuhubiri ujumbe kamili wa Habari Njema za Habari Njema kwamba sadaka ya Kristo na ufufuo wake ulitimiza sheria na nabii za Agano la Kale.

"Na sasa, nikiwa ninamtii Roho Mtakatifu, nakwenda Yerusalemu, bila kufahamu yatakayonipata huko" (20:22)

"Roho Mtakatifu ananionya kwamba vifungo na dhiki vyaningoja lakini siyahesabu maisha yangu kuwa ni kitu cha thamani kwangu, kama kuumaliza mwendo wangu na huduma yangu niliyoipokea (kwa furaha, KJV). Ananitaka kuishuhudia Habari Njema ya neema ya Mungu (ndani ya Yesu) (20:23-24) kwa wengine.

Paulo aliwaonya, "Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi wake ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe"… Najua ya kuwa baada ya kuondoka kwangu watu wabaya wataingia kwenu na kujaribu kubadilisha kweli ya Mungu" (20:28,30).

Roho Mtakatifu aliwachagua viongozi wa kanisa ili wawajibike kwa Mungu, sio kwa Paulo, wakati Paulo alipokuwa tayari kuondoka, watenda kazi wa



4. Unawaalinda vipi Waongofu wapya na mafundisho ya uongo na desturi zinazozuia makusudi ya Mungu (15:30-34)?

**Fikiria kuhusu hili:** Eleza njia za kuwasaidia viongozi wa kanisa (15:10-19), washirika (20-29) na makanisa mengine (23). Ombea makanisa mengine yaje kweli ya Mungu inayowaweka watu huru kutoka kwenyew desturi zisizoweza kuwasaidia. Ombea umoja kwenye mikutano ya kanisa na masiliano ya waumini katika taifa na duniani

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 16

**Jifunze kuhusu:** *Maelezo binafsi ya kazi ya Paulo (1-5); umuhimu wa Roho Mtakatifu katika kazi ya Puklo (6-10); matokeo ya kumtii Roho Mtakatifu (11-15); matokeo ya kukataa msaada wa nguvu za pepo wa uaguzi (16-24); jinsi Paulo na Sila walivyokuwa gerezani (25-30); Paulo alivyoaka heshima ya mamlaka ya kirumi (35-40).*

## SAFARI YA PILI YA PAULO YA KIMISHIONARI

Paulo na Sila walikwenda Derbe na Listra. Kila mahali barua kutoka kwa viongozi wa kanisa la Yerusalemu ilisomwa na waumini walitiwa moyo,

Kule Listra, Paulo alimkuta kijana aliyeitwa Timotheo. Mama yake na bibi yake walikuwa Wayahudi waongofu, waliomwamini Yesu kama Mwokozi wao. (2 Tim. 1:5).

Paulo alimwamini kijana Timotheo akamchukua afuatane nao. Baba yake Timotheo alikuwa Mhunani (hakuwa Myahudi). Kwa vile Timotheo alikuwa hakubaliki na baadhi ya Wayajudi, basi ilimbidi Paulo awatahiri kwa ajili ya Wayahudi (16:3). Torati sio ya lazima katika kuwapatanisha na Mungu (Gal. 2:16), na Paulo alitaka kuonyesha heshima kwa Wayahudi.



**Maono ya Paulo ya Mtu aliye muita Makedonia**

Paulo, Sila na Timotheo waliyatembelea makanisa ya eneo hilo ili kuwatia moyo. Hesabu yao ikaongezeka kila siku (16:5). Baadaye wakaenda kwenye miji ambayo Paulo alikuwa hajaifikia.

Kila siku Paulo alimsubiria Mungu ajue la kufanya. Alienda Galatia kwa sababu Roho Mtakatifu alimkataza asiende KLaskazini. (16:6). Ni muhimu daima tujuenini tusifanye na kipi tufanye.

Usiku mmoja Pulo alitokewa na maono alimwona mtu wa Makedonia akamwita "vuka, uje utusaidie". Asubuhi iliyofuata walitweka kwenda Makedonia (16:10). Paulo na watenda kazi wenzake walimtii Roho Mtakatifu haraka.

Wakati huo, Luka aliungana na Paulo na wenzake mitume ili sisi sote tusome.

Kama Paulo, lazima na sisi tusubiri na kumwamini Roho Mtakatifu atuongoze, na kasha tumtii. Roho Mtakatifu hufanya haya kupitia njia nyingi na mara nyingi:

1. Tunapomwomba Roho Mtakatifu katika maisha yetu (Lk. 11:13).
2. Tunapofanya mambo yampendezayo Bwana (16:5)
3. Tunapowaswhuhudia wengine kuhusu Yesu Kristo (Lk. 21:13-15)
4. Tunapojifunza maandiko ya Nenon la Mungu (2 Tim. 3:16-17)
5. Tunapokuwa tayari na kusubiri kumtii (16:10).
6. Tunaposonga mbele na kazi ya Mungu alivyotuambia tufanye. (16:6)

Paulo alikuwa aafanya yote wakati Roho Mtakatifu aliposema naye na kuwapeleka mbele (16:6-10).

Walisafiri kwa mashua kwenda Makedonia ya kusini.

Hapakuwa na Sinagogi la kiyahudi mjini Philipi; hivyo wakaenda nje ya lango (mji) mpaka kwenye mto; hapa walipata "mahali maalumu kwa kufanyia maombi (16:13). Paulo na wenzake walisema na wanawake waliokutana kando yam to kusali. Tayari walikuwa ulaya, mahali ambapo Wayahudi walikuwa wachache. Hata hivyo, m walijua kuwa Roho Mtakatifualikuwa pamoja nao na akiwaongoza. Huu ulikuwa wakati maalum na mahali mafaka kuzungumzia kuhhsh Yesu.

Mwanamke mmoja mfanya biashara aliyeitwa Lidia aliwasikiliza ukweli ktoka kwa Mungu. Ingawa hakuwa Myahudi, lakini alimwamini Mungu. Akampokea Yesu kama Mwana wa Mungu na akajazwa Roho Mtakatifu. Yeye na familia yake waliamini na kubatizwa na kuwasihi Paulo na wenzake wakae nyumbani wake (16:14-15).

Ilikuwea ni muhimu kwa Paulo, myahudi kujifunza kuwa Mungu huwaita wasichana maskini walio watumwa wamwamini Yesu sawa na wanawake matajiri wafanya biashara.

## MUNGU ANAWAOKOA PAULO NA SILA WATOKE GEREZANI

Mara nyingi mitume walikwenda kusali kando ya mto mahali palipokuwa na ukimya. Siku moja kijakazi mmoja aliyekuwa na pepo wa uaguzi aliwafuata "aliwapatia bwana zake fedha nyingi kwa kuagua na kuwapigia watu ramli (kutabiri mambo yajayo kwa uchawi) (16:16). Watu walimlipa fedha baada ya



mji alijaribu kuwatuliza makutano, akijua kuwa gavana wa Rumi angetaka kujua sababu ya kuwapo fujo katika mji huo (19:35-41). Hivyo Paulo hakuondoka Efeso wakati huo. Alibaki pamoja na waamini. Alitaka kuwasaidia.

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Je, Paulo aliwatiia moyo waumini wapya wa Efeso kwa namna gani (19:4-6)?
2. Kwa nini ni muhimu kuchoma moto au kuteketeza vitu vilivyotumika katika uchawi, uganga na uaguzi wakati tunapoamwamini Yesu (19:19)?
3. Mahubiri ya Paulo yaliathiri vipi ibada za miungu katika mji wa Efeso (19:26)?
4. Mungu alimtumiaje mtu asiyeamini kuwatuliza watu waliokuwa wanafanya ghasia (19:25-41)?

**Fikiria kuhusu hili:** Wafuasi wa Kristo wanaweza kufanya nini ili kutiana moyo? Ni miujiza gani tunaweza kutegemea kuifanya leo kwa jina la Yesu na nguvu za Roho Mtakatifu (19:11-12)?

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 20

**Jifunze kuhusu:** *Jinsi Roho Mtakatifu alivyomwongoza Paulo, (1-7; 11-16); jinsi Paulo alivyowafundisha waumini na kumfufua kijana mdogo (7-11); Paulo alivyojiamini mwenyewe (17-27; 33-35); maneo ya mwisho ya Paulo kwa viongozi wa kanisa la Efeso (28-32); jinsi viongozi wa kanisa walivyoonyesha upendo wao kwa Paulo (36-38).*

## PAULO ANAAMUA CHA KUFANYA

Paulo alijua wakati wakukaa na wakati wa kuondoka. Ingawa Paulo alikuwa mhubiri na mwalimu mwenye shughuli nyingi; lakini alisikiliza uongozi wa Roho Mtakatifu. Aliendelea kukaa na Waefeso mpaka ghasia zilipokwisha tulia. Paulo aliwatia moyo waamini muda wa kuondoka ulipowadia, kisha akaondoka (20:1) kuyatembelea makanisa ya Makedonia na Akaya (Ugiriki) kabla ya kurudi Troa katika Mkoa wa Asia (20:3-6).

Paulo alijua kwamba lazima:

- atimize wito wake wa kiungu wa kuhubiri Habari Njema kwa watu wa Mataifa;
- aongozwe na Roho Mtakatifu ili ajue wakati wa kusonga mbele;
- apande makanisa mapya na kuwafundisha na kuwatia moyo waumini wapya;
- awatii viongozi wake wa kanisa la Antiokia ya Syria, ambao mara kwa mara walimwombea.

Paulo pia alitarajia kutembelea Yerusalemu, Rumi na Spaniola.

Mungu alifanya miujiza mingi kwa mikono ya Paulo hasa ya kuponya wagonjwa na kutoa pepo wachafu (19:11-12). Wana wa kuhani mpagani walikuwa wachawi. Walipomwona Paulo akitoa pepo walijaribu kufanya hivyo pia.

Siku moja walijaribu kumwiga Paulo, walipokuwa wamemwona mtu aliyepagawa na pepo na kusema kwa sauti kubwa "kwa jina la Yesu anayehubiriwa na Paulo, nakuamuru umtoke" (19:13).

Yule pepo akawajibu" Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani (19:15)? Na yule aliyepagawa na pepo mchafu akawarukia wawili na kuwapiga; nao wakakimbia kutoka katika nyumba ile hali wa uchi na kujeruhiwa.

Kwa sababu hiyo watu wengi katika Efeso walioamini wakaja wakaungama kwa ajili ya matendo mabaya waliyofanya. Wakavichoma vitabu vyao na vitu vingine walivyovitumia katika mambo ya uganga "Neno la Bwana likazidi kenea kila mahali"

**Nguvu ya Mungu leo (19:19)**

"Tumeona nguvu ya Mungu ikitenda kazi. Alitutembelea na miujiza. Watu wakaleta sanamu zao kuchomwa moto na kutoa maisha yao kwa kristo. Mawazo ya watu yakabadilishwa kupitia kuhubiri neno la Mungu. Usiku, baadhi yao hawakulala wakarudi asubuhi kukiri mambo mabaya waliyokuwa wamefanya.huu ulikuwa ni wakati wa neema ya Mungu. Sasa huwa ninapokea simu na kutembelewa na watu ili kumsifu Mungu kwa sababu Yeye ameyabadilisha maisha yao. Utukufu kwa Mungu" (Mchungaji B. Burkina Faso, Septemba 2004)

## KAZI YA ROHO MTAKATIFU KATIKA MJI WA EFESO

Kazi ya Roho Mtakatifu katika Efeso ilikuwa ya nguvu sana. Habari njema ilienea kila mahali (19:20)

Katika kipindi hiki Paulo alimaua kuyatembelea makanisa mapya ya Makedonia na Akaya. Aliazimia pia kutembelea Yerusalemu na Rumi (19-21). Yerusalemu ilikuwa kitovu cha dini ya kiyahudi na wafuasi wa Kristo kwa wakati ule pia. Rumi ilikuwa ndio mji mkuu na kitovu cha ngome ya Kirumi. Akaya ilikuwa ndio kitovu cha mji mkongwe wa ngome ya kiyunani. Paulo alijua kuwa hii miji ilikuwa ni sehemu muhimu kuhubiri habari njema za Yesu Kristo na kufundisha na kuwatia moyo waamini wapya.

Paulo akakaa Efeso kwa muda zaidi lakini aliwatuma wawili miongoni mwa wasaidizi wake huko makedonia (19:22). Baadae, Paulo aliungana nao huko (20:1).

Katika kipindi hiki, watu waliofanya sanamu za shaba hapo Efeso waliwashawishi watu kufanya fujo kwa wafuazi wa Kristo (19:23-29). Kalani wa



kusikia yaliyosemwa na yule pepo aliyekuwa ndani ya yule msichana. Watu hawa walisikiliza roho za pepo badala ya kumsikiliza Mungu.

Paulo alikasirika wakati kijakazi huyu alipowafuata akipiga kelele "Hawa watu ni watumishi wa Mungu Aliye Juu" (16:17). Aliongea ukweli lakini Paul alijua ilitoka kwa pepo. Paulo alikuwa mjumbe wa Mungu; kijakazi na roho ya pepo hakuwa. Alitumiwa na wamiliki wake kudanganya watu kuhusu siku zijazo.

Baada ya siku kadhaa, Paulo alizungumza na yule pepo mchafu ndani ya msichana. "Katika jina wa Yesu Kristo nakuamuru utoke kwake!" Wakati huo pepo alimwacha (16:18).

Paulo aliamini kwamba nguvu ya Roho Mtakatifu wa Mungu ni kubwa Zaidi ya nguvu ya pepo wachafu iliyodhibiti. Alijua na kuamini kuwa mamlaka ya Yesu Kristo ni kubwa Zaidi kushinda nguvu ya shetani.

Bwana zake waliona kuwa yule kijakazi alipoteza nguvu zake, na walikasirika, maana hawangeweza kupata fedha tena; kupitia kijakazi uule kwa wauguzi. Ndipo wakawakamata Paulo na Sila waikawakioikota mpaka sokoni. Wakasababisha na kupiga kelele, "watu hawa wanachafua sana mji wetu; nao ni Wayahudi, tena wanatangaza habari ya desturi zisizokuwa halali kwetu kuzipokea wala kuzifuata, kwa sisi tu Warumi" (16:20-21). Huu iuloiliwa ni uongo na hakuwa haki. Viongozi wa mji wakawaamru Paulo na Sila kuchapwa bakora na kuwatupa gerezani. Lakini Mungu huleta Utukufu kwa Jina lake kama tukiendelea kuwaamuru ingawa tunateswa kwa sababu ya Imani yetu.

Kule gerezani, usiku wa manane" Paulo na Sila walipokuwa wakimwimbia nyimbo za kumsifu na kumwomba. Ghafla pakawa tetemeko kuu la nchi, likalitikisa gereza. Yule mlinzi wa gereza akaamka na kuona milango ya gereza

**Mapepo yatii nguvu ya Yesu**

Pepo wachafu au mapepo wanamtambua Yesu Kristo na kujua kwamba yeye ni zaidi yenye nguvu. Lakini wanajaribu kuwahadaa Waumini na wale wanaotafuta ukweli kutoka kwa Mungu. Roho mwovu ndani ya kijakazi alijaribu kumdanganya watu ambao alijua yote kuhusu nguvu za Mungu (Matendo 16:17). Kwa kupiga kelele kutokana na kibali chake kwa Paulo na Sila alikuwa akijishughulisha mwenyewe na kwa mabwana wake waovu - kana kwamba wao ni sawa na mitume.

Paulo hakutaka roho waovu kuzungumza na umati. Hawakuweza kuelewa ni nani alikuwa anasema ukweli. Hatupaswi kudanganywa bali tuwe tayari kuamuru roho za pepo ziondoke kwa jina la Yesu. Usifanye hii peke yako wala kuwagusa watu wenye roho mbaya. Waulize Wakristo wengine kukuombea wewe na pamoja nawe unapoamuru pepo wachafu waende. Kumbuka hilo Yesu aliwatuma wafuasi wake kufanya kazi pamoja wawili wawili (Mk 6:7).

imefunguka. Akadhani kwamba wafungwa wametoroka. Akafuta mpango wake akataka kujiua, lakini Paulo alipaza sauti yake kwa nguvu, akisema, usijidhuru, kwa mana sisi sote tupo hapa". (16:25-26).

## MUNGU ANAMWOKOA MLINZI WA GEREZA

Mlinzi wa gereza alishituka sana kama wafungwa watakuwa wametoroka watawalaa wa kirumi wangemlaumu.

Akapiga magoti mbele ya Paulo na Sila. Akalia". Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka"? Wakamjibu "Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako" (16:16; 30-31). Wakamwambia neno la Bwana, yeye na watu wake wote wakati uo huo". Mlinzi wa gereza akaokoka pamoja na familia yake. Usiku wa manane, akawachukua Paulo na Sila nyumbani kwake, na kuwapa chakula. Hii ilionyesha kuwa alikuwa amebadilishwa.

Paulo alimbatiza mlinzi wa gereza pamoja na familia yake yote. Kwa Paulo na Sila, tendo hili lilikuwa ni muhimu kuliko yote; kutii maneno ya Yesu katika Mathayo 28:19-20" enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi". Mateso yao gerezani hayakuzuia nguvu ya Mungu kutenda kazi.

Kulipopambazuka, makadhi wakatuma wakubwa wa askari wawaachie Paulo na Sila (16.35). Wakawaomba waondoke, (16:39) kwa sababu Paulo alikuwa ni mrumi na ilikuwa kosa kuchapa viboko warumi.

Hadithi hii inaonyesha jinsi tunavyotakiwa kumwamini Mungu katika hali zote na mambo yote. Hadithi hii inatupa picha ya ajabu ya upendo wa Mungu. Hapakuwa na kukamatwa watu au adhabu bali msamaha wa dhambi. Mlinzi wa gereza na wote walioamini walimfuata Yesu, Mwana wa Mungu.

Walipotoka gerezani Paulo na Sila walirudi nyumbani kwa Lidia, wakakaa hapo kwa muda mfupi tu, wakaenda zao kwenye mji uliofuata, walitii wito wa Mungu wa kuhubiri Habari Njema katika Makedonia.

Waumini wa Filipi wakaimarika katika Imani. Walimpenda Paulo na kumpatia mahitaji yake ingawa ni wachache wengine walifanya hivyo (Wafilipi 1:3-5; 4:14-16).

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Kwa nini Paulo alimtahiri Timotheo (16:10)
2. Eleza njia mbili ambazo Roho Mtakatifu alimwongoza Paulo (16:5-9). Je Yeye aliitikiaje (16:10)?
3. Je u a muda maalumu na mahali ambapo huwa unaweza kuomba kwa iukimya kwa Mungu (16:13)?
4. Paulo alijifunza nini kuhusu wito wa Mungu kwa wanaume na wanawake kuhudumia katika makanisa (2:17; 16:1-3,14-15)?



Apolo alitaka kwenda Akaya; na ndugu wote wakakubali na kumuhimiza kwa kuwaandikia wale wanafunzi wa Akaya wamkaribishe. Alipofika huko aliwasaidia sana wale waliokwisha kuamini kwa neema ya Mungu. (18:27).

**Zungumza kuhusu hili:**

1. Ni vizuri kwa viongozi wa kanisa kuwa na kazi za muda ili kujipatia fedha (18:3)?
2. Paulo alikasirishwa na viongozi wa Wayahudi katika mji wa Korintho. Aliamua nini (18:6)?
3. Paulo alijuaje kuwa alikuwa mahali sahihi (18:9-11)?
4. Mungu alimwokoaje Paulo na Wayahudi waliotaka kumletea matatizo (18:12-16)?
5. Kwa nini unafikiri Paulo alisafiri kwenda Yerusalemu, Antiokia ya Syria na Mkoa wa Asia (Galatia na Frigia) (18:22-23)?
6. Ndugu walioamini kule Efeso walimsaidiaje Apolo? Matokeo yake yalikuwa nini (18:27)?

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 19

**Jifunze kuhusu:** *Mafundisho ya Paulo ya ubatizo na Roho Mtakatifu (1-7); huduma ya Paulo katika jiji la Efeso (8-12); matokeo ya kutumia Jina la Yesu bila kuwa na nguvu za Roho Mtakatifu (13-16) kazi ya Roho Mtakatifu kule Efeso (18-20); mipango ya Paulo (21-22), jinsi Mungu alivyowatumia viongozi wa jiji la Efeso kukwepesha ili Paulo asipate shida (23-41)*

## SAFARI YA TATU YA KIMISHIONARI YA PAULO

Paulo aliporudi Efeso, alikutana na wanafunazi kadha wa kadha waliokuwa wamebatizwa na Yohana mbatizaji, baada ya kutubu (19:3). Ndipo Paulo alipowabatiza kwa jina la Bwana Yesu (19:5). Paulo pia aliweka mikono yake juu yao, na kuwaombea (19:6). Roho Mtakatifu akaja juu yao. Baadhi yao wakaanza kunena kwa lugha na wengine kutabiri. Baadhi ya vipawa vya Roho Mtakatifu na Mungu kwa mwamini.

Paulo akanena kwa ushujaa ndani ya Sinagogi kwa miezi mitatu. Wakati baadhi ya watu walipoanza kumpinga na kuitukana ile Njia ya Yesu, Paulo akaenda kwenye kufundisha katika darasa la Tirano kila siku alifundishia pale kwa miaka miwili ili Wayahudi na Wayunani wote waliokaa Asia wasikie neno la Bwana (19:10).

Akiwa Efeso Paulo aliandika nyaraka zake kwa Wakorintho, ambazo zilikuja kuwa sehemu ya Agano Jipya. Akaeleza mafundisho ya Yesu ili kuwazuia wasiziendee njia mbaya katika maisha yao. Aliwimarisha Imani zao na kuwaonya kuhusu mafundisho ya uongo. Paulo alipopanda makanisa, alijaribu kuyaandikia au kuyatembelea.

**Kazi na huduma**

Paulo alikuwa na kazi ya kawaida ya kushona mahema. Aliyauza mahema aliyoyatangza ili kujipatia fedha. Alifanya kazi pamoja na Akila na Prisila kule Korintho (18:3). Tunaamini aliendelea kufanya kazi hii alipotembelea miji mingine. (20:34)

Paulo alishona mahema ili kupata fedha kwa ajili ya kulipia gharama ya chakula na mavazi. Hakuwategemea wengine wampatie fedha kwa ajili ya mahitaji yake. Paulo aliamini ilikuwa vizuri kutumia sehemu ya muda wake akifanya kazi na sehemu ya muda wake akifanya kazi na sehemu ya muda akifundisha na kuhubiri. Kwa jinsi hiyo hakuwa mzigo kwa watu alioishi nao. Hakupokea malipo alipowafundisha, badala yake ndugu walioamini walitoa kwa ajili ya maskini wa Yerusalemu.

Paulo alifanya kazi ya Mungu lakini pia alishona mahema ya kuuza. Alifurahia kufanya yote mawili akiamini kuwa Mungu alimtaka afanye hivyo, Paulo alimpa Mungu utukufu kwa kazi zote alizoweza kuzifanya – kushona mahema, kufundisha na kuhubiri. Alifanya yote haya kwa utukufu wa Mungu.

Walimu wengi wa Biblia, watumishi, wahubiri na wainjilisti wanazo kazi za kulipwa. Baadhi hufanya kazi ya huduma muda wote na wanalipwa na makanisa yao au misheni zao. Wengine hufanya kazi ya kujipatia fedha ikiwa sehemu ya muda wao, na muda mwingine kufanya kazi ya huduma bila malipo. Kazi zote hizo wanazofanya humtukuza Mungu na Yeye hubariki kazi wazifanyazo.

Paulo alipokuwa Korintho, aliwaandikia Wathesalonike nyaraka zake mbili, akiwapongeza, kuwatia moyo na kuwasahihisha. Nyaraka hizo baadae zikawa sehemu ya Agano Jipya.

## PRISILA, AKILA NA APOLO KATIKA MJI WA EFESO

Baada ya muda, Paulo alikwenda Efeso akiambatana na Prisila na Akila. walipofika huko, Paulo aliwaacha akarudi Yerusalemu, na baadae kwenye kanisa la nyumba la Antiokia ya Syria (Shamu) (18:18-22).

Baada ya muda huko Antiokia, Paulo alirudi kwa makanisa ya Galatia na Frygia. 'Akawatia nguvu Waumini wote huko' (18:23).

Baada ya muda kadhaa, Apolo akafika Efeso alikuwa ni maliwa wa Alexandria (18:24) katika nchi ya Misri, kwa vile alikuwa hodari katika maandiko ya Agano la Kale, alianza kunena na kufundisha kwa usahihi kuhusu Yesu. Ila alijua tu kuhusu ubatizo wa Yohana mbatizaji (18:25). Prisila na Akila walimsaidia wakamwelezea njia ya Bwana kwa usahihi zaidi (18:26), ikiwa ni pamoja na mafundisho kuhusu Roho Mtakatifu aliyeahidiwa na Yesu kwa ndugu wote walioamini (1:4-5; 2:38).



5. Lidia alifanya nini ili kuwasaidia wale waliohubiri Habari Njema (16:15-16,40)?
6. Paulo na Sila walifamya nini walipokiwa katika shida (16:25)?
7. Mlinzi wa gereza aliokolewa a nini (16:27-31)? Ni tendo gani la pili alifanya (33-34)?
8. Kwa nini askari wa kirumi walimwogopa Paulo (16:36-40)?

**Fikiria kuhusu hili:** Je, unamwamini Roho Mtakatifu kukuonya usiende njia mbaya na badala yake kukuongoza kwa watu ambao wanahitaji kujua kuhusu Yesu (16:7,10)? Matokeo ya kutii Roho Mtakatifu yalikuwa yapi? (16:11-15) na kukataa msaada kutoka kwa nguvu za roho waovu (16:16-24)? Ombea viongozi wa kanisa wawe wazi kwa uongozi wa Roho Mtakatifuna wazitambue roho zidanganyazo.

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 17

**Jifunze kuhusu:** *Njia ya Paulo ya kuwahubiria Wayahudi na Mataifa (1-3,10-11); jibu la viongozi wa kiyahudi (5-9,13-15); jibu la kawaida kwa mahubiri ya Habari Njema (4,12); sababu za mwitikio hafifu kule Athene (16-34).*

## PAULO ANAHUBIRI KUTOKA MJI HADI MJI

Paulo na rafiki zake wakienda Thesalonike katika Sabato tatu Paulo aliingia kwenye Sinagogi la Wayahudi; akawafundisha akithibitisha kutoka kwenye Agano la Kale "kwamba Masihi ilibidi kuteswa na kufufuka katika wafu. Yesu huyu ninayewapasha habari zake ndiye Kristo (Masihi) (17:3)**.** Baadhi ya Wayahudi waliamini. Pia wengi waliamini.

Yasoni, mwamini wa Kiyunani aliwakaribisha nyumbani kwake. Viongozi fulani wa Wayahudi wakaona wivu, kwa Yasoni wakiwatafuta Paulo na Sila kwa vile hawakuwaona wakamkokota Yasoni mbele ya wakubwa wa mji wakipiga kelele wakisema, "watu hawa walioupindua ulimwengu wamefika huku nako; na Yasoni amewakaribisha. Hawa wanatenda mambo yaliyokinyume na Kaisari, wakisema kwamba yupo mfalme mwingine, aitwaye Yesu" (17:6-7).

Yasoni akalipa fedha ya dhamana, akaachiliwa. Usiku ulipowadia, hao ndugu wakawapeleka Paulo na Sila mpaka Beroya.

Kwa usalama wao. Kule Berea, Wayahudi wengi walipokea ujumbe wao. Walijisomea Agano la Kale kwa makini na kwa uangalifu kila siku. (17:11). Ni muhimu kuchunguza mahubiri na mafundisho yote na Neno la Mungu. Wayahudi hao pia wakafunguka mawazo yao na kuyaeleza maandiko ya Roho Mtakatifu. Wayahudi na Wayunani wengi, wanaume na wanawake, wakaamini (17:12). Lakini Wayahudi wenye wivu waliwafuata huko Berea, pia ili wapate kuwasumbua waliohubiri Habari Njema. Ndugu wakawapeleka Paulo na Sila mpaka Athene, mji mkuu wa Ugiriki.

## NI WATU WACHACHE TU WANAAMINI KULE ATHENE

Athene ulikuwa kituo cha utambaduni na kujifunza wakati wa Paulo. Alichukizwa sana alipoona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu. Akahubiri Habari Njema kuhusu Yesu na ufufuo wake. Katika Sinagogi alihojiana na wale waliomwabudu Mungu mmoja wa kweli (17:17). Akawaeleza jinsi Yesu alivyokuwa Masihi wao. Pia alizungumza na watu waliokutana naye sokoni kuhusu Yesu.

Wanaume fulani wakamshika, wakamchukua Aeropago, mahali mahakama ilipokutana. Wakamweleza "Je, twaweza kujua maana ya elimu hii mpya" (17:19)?

Wayunani walikuwa na sanamu nyingi, lakini hawakumjua Yahweh; Mungu mmoja wa kweli na Aliye Hai nan a Yesu Kristo Mwana wake. Paulo alishirikiana nao kuhusu Imani yake kama ifuatavyo: -

1. Mungu mmoja wa kweli aliufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo "Yeye hakufanyika kwa mikono ya wanadamu (17:24).
2. "Mungu hahitaji kitu chochote" Yeye ni Mungu Mwenyezi, Muumbaji wa ulimwengu anayetoa uzima na pumzi na vitu vyote, (17:25). Yeye ni Bwana wa vitu vyote
3. Watu wote duniani wametoka kwa mtu mmoja (Adamu) aliyemwumba (17:26)
4. Mungu aliamua na kuwawekea nyakati na mipaka ya makazi yao (17:26). Mungu alifanya hivyo ili tumtazame Yeye aliye Mungu mmoja wa kweli, tukamwone na kumtafuta kwa vile Yeye hawi mbali na kila mmoja wetu (17:27).
5. Mungu ndiye aliyeumba uzima na hivyo tunaishi kwa sababu Yake, maana sisi sote tu wazao wake (17:28).
6. Mungu hakutokana na dhahabu, fedha au jiwe. Hivyo hatupaswi kumdhania hivyo na kumwabudu tukimfananisha navyo.
7. Sasa Mungu anaagiza watu mtubu na kuziacha dhambi zenu na Imani zenu potofu (17:30)
8. Mungu alimtuma Mwanae ili sisi katika Yeye na siku ya mwisho Mungu atatuhukumu (17:31, Yoh. 3:17,12:48).

Baada ya Myunani kusikia kuhusu Yesu kwamba alifufuliwa kutoka wafu, baadhi yao walicheka (kufanya dhihaka). Wengine walimwambia, "Tutakusikiliza tena katika habari hiyo" (17:32)**.**

Watu wa Athene walikuwa matajiri, werevu na wenye elimu ya juu. Walipenda tofauti. Hata hivyo, watu wengi hawakumwamini Mungu mmoja wa kweli na Mwenyezi na Mwana wake Yesu Kristo. Baadhi yao waliamini, wakiwemo Dionisi, na mwanamke mmoja jina lake Damari. (17:34).



**Zungumza kuhusu hili:**

1. Watu walifanya nini Paulo alipohubiri Habari Njema za Yesu Kristo kule Thesalonike (17:32-34)?
2. Nani alimwamini Yesu (17:4,12,34)?
3. Ni mambo gani Paulo alioyajumuisha alipozungumza na watu wasioamini kuhusu Kristo (17:24-31)

## Kusoma Biblia: Matendo Sura ya 18

**Jifunze kuhusu:** *Kwa nini Paulo alijitoa kushona mahema alipokuwa Koritho (1-3); kwa nini Paulo aliacha kuwahubiria Wayahudi (4-7), kwa nini Paulo alikaa muda mrefu korintho (8-17); Paulo aliyatia moyo vipi makanisa (18-23); ndugu au waumini walitiana moyo kwa namna gani (24-28).*

## MUNGU ANAMTIA MOYO PAULO AHUBIRI KATIKA MJI WA KORINTHO

Paulo hakukaa Athene kwa muda mrefu. Aliende koritho akaishi nyumbani kwa Akila na Prisila mke wake, ambao walikuwa mafundi wa kushona mahema. (18:1-3). Wakati huo, Klaudio alikuwa mfalme wa Rumi. Viongozi wa Wayahudi kule waliwasumbua wote waliomwamini Kristo kama Masihi; hivyo akawaamuru ndugu wote waaminio watoke Rumi kwa vile Akila na Prisila walikuwa Wayahudi waliomwamini Yesu, iliwabidi waondoke Rumi; wakaenda kuishi Korintho; mahali Paulo alipowakuta; akaishi kwao na kushona mahema kwa pamoja ili kujipatia fedha. Baadae Akila na Prisila walikwenda kuishi Efeso, ambako ndugu walioamini walikutana kama Kanisa, ndani ya nyumba yao (1 Kor. 16:19).

Sila na Timotheo walikuja katika Makedonia kujiunga nao huko Korintho huo wakati huo Paulo alitumia muda wake wote akihubiri, akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo (18:5).

Walipopingana naye na kumtukana Mungu, Paulo alikasirika (18:5-6), akaamua kwenda kuwahubiri watu wa Mataifa tu.

Muda mchache baadae, Mungu akasema na Paulo kwa maono akimwambia, "usiogope, bali nena, usinyamaze; kwa kuwa niko pamoja nawe wala hapana mtu atakaye kushambulia ili kukudhuru. "Mungu alikuwa na watu wengi katika mji wa Korintho ambao wataamini Habari Njema za Yesu na kuokolewa (18:9-10). Hivyo Paulo akakaa huko kwa mwaka mmoja na miezi sita akiwafundisha kutoka kwenye neno la Mungu [katika Agano la Kale] (18:11).

Wayahudi wakimwinukia tena Paulo, kwa nia na kumpeleka mbele ya Galio, Liwali wa kirumi wa Akaya kwa kuhukumiwa. Lakini Liwali Galio hakuwasikiliza Wayahudi (18:12-16).